View metadata, citation and similar papers at core.ac.uk

brought to you by CORE

provided by Digital Library of Open University of Tanzania

# KUTATHIMINI MBINU ZA UFUTUHI KATIKA KUELIMISHA JAMII KUHUSU JANGA LA UKIMWI KATIKA TAMTHILIYA YA EMBE DODO NA USHUHUDA WA MIFUPA

**LUCY CHAKUPEWA GWANKO**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2017**

## UTHIBITISHO

Mimi, Prof. Emmanuel Mbogo, nathibitisha kwamba nimeisoma tasnifu hii iitwayo: *"**Kutathimini Mbinu za Ufutuhi Katika Kuelimisha Jamii Kuhusu Janga la Ukimwi, katika tamthiliya ya Embe Dodo ushuhuda wa mifupa*** nimeridhika kwamba imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuwasilishwa kwa ajili ya Utahini wa Shahada ya Uzamili ya Fasihi kwa Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…………………………………………

**Prof. Emmanuel Mbogo**

**(Msimamizi)**

…......................................………..

Tarehe

# HAKIMILIKI

Tasnifu hii au sehemu yake yoyote hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa, Kubadilishwa au kuhaulishwa kwa mbinu yoyote ile: kielektroniki, kimekanika, kunakilishwa, kurudufiwa, kupigwa picha, au kurekodiwa kwa utaratibuwowote ule katika hali yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wake au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, kwa niaba yake.

## TAMKO

Mimi **Lucy Chakupewa Gwanko**, nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Shahada yoyote.

………………………………...................

Saini

………………………………….........

Tarehe

# TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa baba yangu mzazi Zakayo Chakupewa Gwanko na mama yangu Olipa Chakupewa Gwanko, mme wangu Livingstone Fidelis na watoto wetu wapendwa Layson, Lulu na Leonata Livingstone, pia bila ya kuwasahau wataalamu na wanafunzi wote wa fasihi ya Kiswahili.

## SHUKRANI

Katika mafanikio yoyote, upo mchango wa kimawazo, kifedha ama kiutendaji na kwa sababu mafanikio ya kazi hii sikuweza kujitegemea mwenyewe kwa kila kitu, inanipasa kutoa shukrani zangu za pekee kwa watu ama taasisi zilizonifanikisha katika malengo yangu. Nikianza na shukrani za pekee kwa yeye anayetupatia pumzi ya uhai na kutupatia riziki kubwa kubwa na ndogo ndogo ambaye ni Mwenyezi Mungu kwani katika mafanikio haya si kwa nguvu zangu bali ni kwa neema yake.

Wapo watu ambao inanipasa kuwafanyia iliyo haki kwa kuwataja katika kufanikisha katika tasnifu hii; shukrani za pekee kwa mwalimu na Msimamizi wangu Prof. Emmanuel Mbogo kwa juhudi zake alizonifanyia kwa kusimamia na kuisahihisha kazi hii hadi kufikia ubora huu, hakika anapaswa kuheshimiwa kwa mchango wake na anastahili kuigwa kwa mazuri haya. Naweza kumbuka maneno yake ya kutia moyo ambayo mara nyingi alikuwa akiyatumia, ‘tusikate tamaa’ neno hilo lilikuwa likinitia moyo sana kwani alikuwa ananiambia mara nyingi kuwa ukiwa na mimi hauwezi choka. Mengi yaliyo katika kazi hii ni sehemu tu ya matunda ya ujuzi wake mkubwa na ushauri wake wa kitaalamu. Ninapenda pia kumshukuru Prof. Emmanuel Mbogo kwa kunifanikisha katika kukamilisha tasnifu hii, kwani amekuwa akinitia moyo na kutoa muda wake mwingi kunielekeza kwani mara nyingi nilitaka kufahamu undani wa kazi yake ya tamthiliya ambayo nimeitumia katika kazi hii. Siwezi kuwasahau wasanii wa kazi ya kifasihi ziitwazo *Embe dodo* ya D.Z.Makukula na *Ushuhuda wa Mifupa* ya Ibrahim Ngozi] kwani walikubali kutoa mawazo yake yaliyokamilisha kazi hii akiwa kama mtafitiwa, naomba Mwenyezi Mungu ambariki sana.

**IKISIRI**

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza mbinu za ufutuhi katika kufikisha maudhui katika tamthiliya kwa kulinganisha kazi mbili za tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* ili kubaini mbinu za ufutuhi zinavyowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala la ugonjwa wa ukimwi na njia za kuenea kwa ugonjwa wa ukimwi. Utafiti huu ulitumia mbinu moja ya ukusanyaji data ambazo ni; maktaba. Aidha data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi linganishi. Utafiti huu uliongozwa na *Nadharia ya Elimumitindo katika Uchambuzi wa Matini za Kifasihi*. Utafiti umegundua kuwa, tamthiliya hizi zinatofautiana katika mbinu za kisanii na ubunifu. Tamthiliya ya *Embe dodo* imetumia mbinu za ufutuhi ubeuzi zaidi wakati tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* imetumia mbinu ya ufutuhi uzimbwe zaidi, rahisi na ya wazi zaidi. Aidha utafiti huu umebaini kuwa, tamthiliya hizi zinatofutiana katika kuwasilisha suala la ugonjwa wa ukimwi na njia za kuenea kwake katika jamii ya Tanzania katika vipindi viwili tofauti. *Embe dodo* anawasilisha suala la mila na desturi linavyopingana na njia za kujikinga na ugonjwa wa ukimwi wakati *Ushuhuda wa Mifupa* inajadili kwa uhalisia juu ya njia mbali mbali ambazo zilisababisha zaidi kuenea kwa ugonjwa wa ukimwi, ambazo ni ujinga, umaskini na jamii kutokujali. Kwa upande mwingine, ilibainika kuwa tamthiliya hizi kwa vile zimeandikwa na wasanii wa jamii moja ambao wameshuhudia na kupata kuona na masimulizi ya historia ya jamii yao juu za ugonjwa wa ukimwi. Wasanii hawa wanafanana katika kuwasilisha maudhui ya kazi zao ambapo wote kwa pamoja wanajadili juu ya mambo mbalimbali yaliyopo katika jamii kama vile; rushwa, harakati za ukombozi, usaliti, mfumo dume, nafasi ya mwanamke, suala la ugonjwa wa ukimwi.

## YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ...................................................................................... **ii**

**HAKIMILIKI** ...................................................................................... **iii**

**TAMKO** ...................................................................................... **iv**

**TABARUKU** ......................................................................................**v**

**SHUKRANI**...................................................................................... **vi**

**IKISIRI** ...................................................................................... **vii**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ...................................................................... **xi**

**SURA YA KWANZA**......................................................................................**1**

**1.0 UTANGULIZI** ......................................................................................**1**

1.1 Utangulizi......................................................................................1

1.2 Historia Fupi ya Watunzi wa Tamthilia ya Embe Dodo na Ushuhuda wa Mifupa......................................................................................1

1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti......................................................................................2

1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti......................................................................................5

1.5 Malengo ya Utafiti......................................................................................5

1.5.1 Lengo Kuu ......................................................................................6

1.5.2 Malengo Mahususi ......................................................................................6

1.6 Maswali ya Utafiti ......................................................................................6

1.7 Umuhimu wa Utafiti......................................................................................6

1.8 Mipaka ya Utafiti......................................................................................7

1.9 Matatizo ya Utafiti......................................................................................7

1.10 Muundo wa Tasnifu......................................................................................8

1.11 Hitimisho ........................................................................................8

**SURA YA PILI ........................................................................................9**

**2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA .......9**

2.1 Utangulizi........................................................................................9

2.1.1 Futuhi........................................................................................9

2.1.2 Maandiko Yahusuyo Ufutuhi........................................................10

2.1.3 Dhima ya Futuhi........................................................................14

2.1.4 Futuhi wakati wa Ukoloni............................................................19

2.1.5 Futuhi Wakati Ww Sasa Nchini Tanzania......................................20

2.2 Pengo la Maarifa ........................................................................21

2.3 Kiunzi cha Nadharia ....................................................................21

2.3.1 Dhana ya Nadharia ....................................................................22

2.4 Nadharia ya Fasihi Linganishi ......................................................23

2.5 Nadharia ya Elimu Mitindo ..........................................................25

2.6 Hitimisho ....................................................................................27

**SURA YA TATU........................................................................................29**

**3.0 MBINU ZA UTAFITI ........................................................................29**

3.1 Utangulizi......................................................................................29

3.2 Mkabala wa Utafiti........................................................................29

3.3 Eneo la Utafiti ..............................................................................29

3.4 Mbinu ya Usomaji wa Maktabani ..................................................30

3.5 Matini.............................................................................................30

3.6 Uchambuzi wa Data ......................................................................31

3.7 Hitimisho .......................................................................................31

**SURA YA NNE ........................................................................................................33**

**4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ...................................33**

4.1 Utangulizi........................................................................................33

4.2 Uteuzi na Matumizi ya Mbinu za Ufutuhi ....................................................33

4.2.1 Mbinu za Ufutuhi Katika Tamthiliya ya Embe Dodo ..................................33

4.2.2 Mbinu za Ufutuhi katika Ushuda wa Mifupa ..............................................39

4.3 Kulinganua na Kulinganisha Uteuzi wa Mbinu za Ufutuhi Katika Kuwasilisha Ueneaji wa Ukimwi .........................................................................51

4.3.1 Kutofautiana...................................................................................51

4.3.2 Kufanana........................................................................................53

4.3.3 Sababu za Kufanana na Kutofautiana Kwa Mbinu za Ufutuhi ......................54

4.3.4 Hitimisho .......................................................................................55

**SURA YA TANO .....................................................................................................57**

**5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..............................57**

5.1 Utangulizi........................................................................................57

5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti................................................................57

5.3 Hitimisho .......................................................................................60

5.4 Mapendekezo ..................................................................................61

**MAREJELEO .......................................................................................................63**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 2.1: Mbinu za Ufutuhi............................................................................16

Jedwali Na 4.1: mbinu za Ufutuhi katika Embe dodo na Ushuhuda wa Mifupa .......50

# SURA YA KWANZA

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura hii ni sura tangulizi ambayo imetoa usuli wa tasnifu hii. Katika kubainisha tatizo la usuli wa tatizo na tatizo lililofanyiwa utafiti. Sura hii inahusu usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na hitimisho.

## 1.2 Historia Fupi Ya Watunzi wa Tamthilia ya Embe Dodo na Ushuhuda wa Mifupa

Kabla ya kuanza tupate historia fupi ya mtunzi wa tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa.* Tamthiliya ya *Embe dodo* imeandikwa na Dominicus Z. Makukula (2015) ni mzaliwa wa nchi ya Tanzania katika mkoa wa Ruvuma. Tamthiliya ya *Embe dodo* imeandikwa katika malengo ya kuwashawishi Watanzania kubadili tabia au kutumia kinga katika kupambana na ugonjwa wa Ukimwi. Mchezo huu ulichezwa kwa mara ya kwanza na wanachuo mbali mbali katika Chuo cha sanaa Bagamoyo kati ya mwaka 2000 hadi 2005 kwa ubunifu mkubwa wenye matukio ya kufurahisha na kuelimisha. Wakati tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* imeandikwa na Ibrahim Ngozi (1990) iliyolenga kuhamasisha au kufanya kampeni dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi. Kampeni hii ililengwa kuwa ya kudumu katika maisha ya Watanzania ili kuwaweka wananchi kuwa makini au kujihadhari na ugonjwa wa Ukimwi. Hizi ni juhudi za kupambana na ugonjwa wa Ukimwi ambao hauna tiba na dunia nzima ingali ikitafuta dawa za ugonjwa huu hatari, aidha watu wengi wa

vijijini bado hawajaufahamu vyema ugonjwa huu wa Ukimwi. Kazi hii imeangalia kuhusu mchango wa ufutuhi katika uelimishaji wa jamii yetu ya Kitanzania juu ya kupambana na ugonjwa wa Ukimwi, nanma ya kujikinga, unavyoenezwa na nanma ya kuwahudumia watu waliopatwa na ugonjwa huo. Tumechunguza jinsi waandishi hawa walivyotumia ufutuhi katika kuwasilisha suala la ugonjwa wa Ukimwi katika jamii ya Tanzania. Tamthiliya hizi mbili zilichanguliwa kwa sababu zote zinazungumzia ugonjwa wa Ukimwi unavyoambukizwa na namna ya kujikinga nao, tena zimeandikwa na waandishi wawili tofauti. Aidha, tamthiliya hizi zimechaguliwa kwa sababu zote zimetumia mbinu ya ufutuhi katika kuwasilisha suala la ugonjwa wa Ukimwi.

## 1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Tatizo la Ufutuhi ni kutaka kutathimini mbinu za kifutuhi zilivyotumika katika kuelimisha jamii kuhusu janga la Ukimwi. Mtunzi yeyote kwa kazi ya fasihi hutumia ubunifu au ujuzi fulani ili kuwasilisha ujumbe katika jamii husika. Hivyo basi, Ufutuhi ni mbinu iliyotumiwa na waandishi wote wa tamthiliya ya *Embe dodo* iliyoandikwa na Makukula,D.Z (2015) na tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* iliyoandikwa na Ngozi,I (1990). Tamthiliya kama ilivyofasiliwa na Wamitila (2002) ni kazi ya kimantiki na kimaongezi ambayo hutendwa mbele ya hadhira. Anaendelea kusema kwamba, ni tamthiliya ya kimuundo imegawanyika katika matendo na utendaji, mazungumzo ya kusemwa huchukua nafasi kubwa katika uwasilisha ujumbe. TUKI, (2013:538), wanaeleza kuwa, Tamthiliya ni utungo wa kisanaa ambao huweka wazo Fulani katika matendo na mazungumzo, agh.huweza kuigizwa. Hivyo tamthiliya ni utanzu wa fasihi ambao hutendwa jukwaani mbele ya hadhira na

yaweza kuwa katika maandishi mfano *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*. Tatizo hili la ugonjwa wa Ukimwi kwa sasa ni tatizo kubwa katika nchi yetu ya Tanzania. Katika kuthibitisha hilo kuwa ni tatizo kwa sasa, kuna waandishi kadhaa ambao wameandika tamthiliya zao juu ya ugonjwa wa Ukimwi, baadhi yao ni Medical Aid Foundation (2005) *Kilio chetu*, Jilala (2003) *Giza*,Mapalala (2006) Passed *like a shadow* na Steve (2007) *Orodh*a.

Tamthiliya hizo na zingine ambazo hatujazitaja katika utafiti wetu zote zinaongelea juu ya ugonjwa wa Ukimwi na njia za kuenea kwa ugonjwa huo. Hivyo idadi hiyo ya vitabu ambavyo tumeviorodhesha, vyote kuongelea suala moja, ni ushahidi tosha uliomsukuma mtafiti kufanya utafiti wake katika tamthiliya za Embe dodo na Ushuda wa Mifupa ambavyo navyo vinaongelea suala ugonjwa wa Ukimwi.

Kazi hii inahusu Ufutuhi au ucheshi,hivyo tunalazimika kuelezea maana ya futuhi kwa vile ndicho kiini cha utafiti wetu. Tunaomba kukazia kwamba,futuhi havina lengo la kuchekesha peke yake lakini ucheshi huo unaopatikana katika futuhi umekusudia kutoa ujumbe mbali kwa jamii, kama tutakavyoona katika kipengele cha dhima ya futuhi. Dhana ya Ufutuhi imeelezwa na wataalamu mbali mbali kwa njia ya kukaribiana; Senyamanza,(h.t:76), akinukuu Oxford Dictionary: Thesaurus and Wordpower Guide (2007),anaeleza kuwa, neno futuhi wamalifafanua kwa mitazamo mitatu;

i) *Entertainment consisting of jokes and sketches intended to make an audience laugh.*
ii) *A film, play or programme intended to arouse laughter.*
iii) *A humorous of satirical play in which the characters ultimately triumph over adversity.*

Tafsiri

i) *Ni kiburudisho ambacho hujumuisha utani na vibonzo kwa lengo la kuchekesha hadhira.*
ii) *Ni filamu, mchezo wa kuigiza au vitendo ambavyo hulenga kuibua ucheshi.*
iii) *Ni mchezo wa dhihaka unaojumuisha vichekesho, kejeli ambao hatima yake ni kuibua furaha kwa wahusika.*

Maelezo haya yanabainisha wazi kuwa futuhi ni kazi ya kisanaa ambayo imebuniwa ili kuleta furaha au ucheshi miongoni mwa wanajamii au hadhira inayotazama mchezo husika.

FUTUHI

Senyamanza (h.t) anasema; "Lengo la msingi la futuhi ni kuchangamsha na huishia kwa namna ya kufurahisha. Lazima tukumbuke kwamba, kusema futuhi inafurahisha haina maana kuwa dhamira yake haina uzito. Utuhi huweza kuwa na sifa zinazotofautiana, jambo ambalo hutumiwa kama kigezo cha kuainisha aina mbali mbali za ucheshi. Lakini, vyovyote iwavyo, futuhi hujikwepesha na maswala ya kuhuzunisha au kushtua".

Kwa mujibu wa utafiti huu, ufutuhi ni mchezo wa kuigiza au tamthiliya ambao huyaweka mawazo mbali mbali katika matendo ili yaweze kuigizwa katika mtindo wa kuchekesha au kushangaza ili jamii iweza kupata ujumbe uliokusuiwa. Wamitila (2002) anasema, tofauti na katuni, Ufutuhi ambao kwa Kiingereza ni comedy inatokana na neno Komos la lugha ya Kiyunani likimaanusha sherehe za matambiko ya watu wa Uyunani ya kale ambapo watu walifurahi kugonga ngoma kwa kucheza ngoma, kuimba na kutamba majigambo ili kumshukru Mungu wao aitwaye

Dionysius ambaye alikuwa mungu wa rutuba na mavuno . Hivyo katika utafiti huu umeliangalia suala Ufutuhi linavyojitokeza katika tamthiliya hizo mbili na watafiti watabainisha ujitokeza wa matukio ya ufutuhi katika tamthiliya zote mbili na kubainisha maudhui au ujumbe uliobebwa na Ufutuhi huo katika tamthiliya hizo.

## 1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuelezea suala moja katika jamii kwa kutumia ubunifu wa namna mbali mbali. Ingawa wataalamu wanaeleza kuwa kila mwandishi ana namna yake ya kuwasilisha ujumbe kwa jamii yake. Waandishi wanaweza kuwa wawili au zaidi na wakaongelea suala lile lile, lakini wakatofautiana namna ambavyo kila mmoja anavyowasilisha ujumbe wake kwa jamii. Hivyo basi bado kuna haja ya kujua kuwa mwandishi wa tamthiliya za Ufutuhi wanaweza kutumia mbinu zile zile au tafauti katika kufikisha ujumbe kwa jamii kwa kutumia Ufutuhi?(uchekeshaji). Ubainishaji wa mbinu za kifutuhi na kunafanana ama kutofautiana kwa mbinu hizo za Ufutuhi. Hivyo basi tatizo la utafiti ni kwamba tamthiliya nyingi za Ufutuhi hazijafanyiwa uchunguzi wa kina na kuweka bayana jinsi mbinu za Ufutuhi zinavyoweza kubainishwa katika uwasilishwaji wa ugonjwa wa ukimwi kwa jamii husika. Waandishi wawili tofauti wa tamthiliya za *Embe dodo* na *Ushuhuda wa mifupa* wanaweza kuwa na mbinu zile zile au zikatofautiana katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa mifupa?*

## 1.5 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu na malengo mahsusi kama ifuatavyo:

### 1.5.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti huu kulinganisha mbinu za kifutuhi zilivyotumika katika kuelimisha jamii ya Watanzania kuhusu janga la ugonjwa wa Ukimwi katika tamthiliya za Ufutuhi za *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*

### 1.5.2 Malengo Mahususi

Utafiti huu una malengo mahususi mawili:

i) Kubainisha mbinu za kifutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa.*

ii) Kulinganisha na kutofautisha mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa.*

## 1.6 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unajibu maswali yafuatayo:

i) Ni mbinu zipi za kifutuhi zilizotumika katika Embe dodo na Ushuhuda wa Mifupa?

ii) Kuna kulingana na kutofautina gani katika mbinu za ufutuhi zilizoonekana katika tamthiliya ya Embe dodo na Ushuda wa Mifupa?

## 1.7 Umuhimu wa Utafiti

Umuhimu wa utafiti huu umejikita katika nyanja kuu tatu; kwanza, matokeo ya utafiti huu yataongeza maarifa katika nadharia na mbinu za utunzi wa tamthiliya hususani tamthiliya za Ufutuhi wa tathiliya za Kiswahili. Pili, utafiti huu utatoa mchango katika maarifa ya taaluma ya fasihi linnganishi. Hivyo basi, utafiti huu

utaweza kutumiwa kama marejeo, hususani katika fasihi linganishi. Kwa maana hiyo, utawasaidia wanafunzi na watafiti wengine kupata marejeo kuhusu fasihi linganishi na tamthiliya Ufutuhi ya Kiswahili kwa ujumla wake. Tatu, utafiti huu pia utakuwa ni changamoto kwa watafiti wengine kufanya utafiti kuhusu tamthiliya za Kiswahili hususani tamthiliya za Ufutuhi zilizoandikwa na waandishi wawili tofauti na vilevile utatajirisha maktaba ya chuo.

## 1.8 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kuchunguza na kulinganisha ujumbe uliojitokeza katika tamthiliya za kifutuhi. Zipo tamthiliya nyingi zenye kuongelea tatizo la ugonjwa wa Ukimwi, kama vile *Orodha ya Steve Rynolds*,(2007), *Kilio chetu* ya Medical Aid Foundation(2005), *Giza* ya Jilala,(2003),hatukuweza kuzishughulikia tamthiliya zote hizo za ufutuhi. Utafiti huu utajikita katika kubainisha vipengele vya ufutuhi ambavyo ni kejeli,ubeuzi,vijembe, dhihaka na utani katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa mifupa*. Aidha utafiti huu umejikita katika kubainisha tofauti na kufanana kwa mbinu za Ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo ya* Dominicus Makukula na *Ushuda wa Mifupa ya* Ibrahim Ngozi tu kwasababu ndivyo mtafiti alivyovilenga.

## 1.9 Matatizo ya Utafiti

Katika utafiti huu, mtafiti alikutana na matatizo kadhaa ambayo yameifanya kazi ya kiutafiti kuwa ngumu, ila alijitahidi kuyatatua. Tatizo moja lilikuwa upatikanaji wa kitabu cha tamthiliya cha ushuhuda wa mifupa cha Ibrahimu Ngozi. Kitabu hiki hakijaenea sana katika maduka ya vitabu ya mikoa mingine,tofauti na Dar es Salaam

na hata maktabani hakipatikani na hata wanafunzi wa sekondari hawakisomi kama kitabu cha kiada. kitabu hiki ni cha zamani, hivyo mtafiti amekipata kutoka kwa mwanafunzi aliyetunza kopi ya kitabu hicho katika Chuo kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam akapata nakala, ambayo imenisaidia katika utafiti huu. Tatizo la pili, ni upatikanaji wa pesa,kazi zote za kitafiti zitahitaji fedha za kutosha, hivyo mtafiti alilazimika kukopa fedha katika banki ili kukamilisha utafiti huu. Hivyo, ilikuwa ni kazi ngumu kwa mtafiti kukamilisha utafiti huu.

## 1.10 Muundo wa Tasnifu

Muundo wa utafiti huu umegawanyika katika katika sura tano, sura ya kwanza inahusu utangulizi wa jumla wa utafiti, masuala yanayohusiana na tatizo lililofanyiwa uchunguzi katika utafiti huu, yamejadiliwa na kutolewa maelezo ya kina. Sura ya pili inahusu utalii wa kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, ambapo sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Katika sura hii, imeonesha mbinu ya usomaji wa maktabani. Sura ya nne, inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data na sura ya tano, ambayo ndiyo sura ya mwisho, inahusu muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo.

## 1.11 Hitimisho

Sura hii imejadili juu ya usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti, masuala ya kimaadili na muundo wa tasnifu. Aidha katika sura hii ya kwanza tatizo la utafiti litakuwa limebainishwa na kuelezwa wazi na kwa undani zaidi. Sura inayofuata ni sura ya pili, ambayo inahusu Mapitio ya kazi tangulizi na Kiunzi cha Nadharia.

# SURA YA PILI

# 2.0 MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inatalii mapitio ya maandiko tangulizi, katika sura hii maandiko na tafiti mbalimbali zinazohusiana na mada ya utafiti zitajadiliwa kwa kina na hatimaye kuibua pengo la maarifa ambalo liliweka msukumo kufanya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne ambapo sehemu ya pili inahusu dhana ya fasihi linganishi, sehemu ya kwanza inajadili juu ya dhana ya Ufutuhi , ya tatu ni pengo la kimaarifa na sehemu ya nne kiunzi cha nadharia.

### 2.1.1 Futuhi

Senyamanza,(h.t:77-78), akiwanukuu Kennedy na Gioia, (2007: 1257), anaeleza kuwa, Futuhi / Komedia (comedy) linalotokana na neno Komos la lugha ya Kiyunani. Komos linamaanisha sherehe za matambiko ya jamii ya watu wa Uyunani ya kale katika sherehe, sherehe hizo watu walifurahi na kuimba, kucheza ngoma na kutamba majigambo ili kumshukru mungu wao aitwaye Dionysius ambaye ni mungu wa rutuba na mavuno. Wamitila, (2003) anaelezea kuwa, futuhi ni dhana ya ucheshi inayotumia kuelezea uwezo wa kazi ya fasihi na sanaa ya maonyesho kusababisha vichekesho kwa msomaji au mtazamaji.

Senyamanza,(h.t:76), akitoa maelezo katika, Oxford Dictionary: Thesaurus and Wordpower Guide (2007),anasema kuwa, neno futuhi wamalifafanua kwa mitazamo mitatu;Entertainment consisting of jokes and sketches intended to make an audience

laugh.A film, play or programme intended to arouse laughter, a humorous of satirical play in which the characters ultimately triumph over adversity.

Tafsiri; Ni kiburudisho ambacho hujumuisha utani na vibonzo kwa lengo la kuchekesha hadhira.Ni filamu, mchezo wa kuigiza au vitendo ambavyo hulenga kuibua ucheshi. Ni mchezo wa dhihaka unaojumuisha vichekesho, kejeli ambao hatima yake ni kuibua furaha kwa wahusika.Maelezo haya yanabainisha wazi kuwa futuhi ni kazi ya kisanaa ambayo imebuniwa ili kuleta furaha au ucheshi miongoni mwa wanajamii au hadhira inayotazama mchezo husika.

Mbogo, (2015:11), katika nukuu za darasani, anaeleza kuwa, futuhi au Komedia ni utungo ambao unachekesha na kuchangamsha. Tamthiliya ya aina hii inaweza kutusawiria picha yakini katika maisha yetu kwa undani ikitumia dhihaka na kejeli kwa kuchekesha. Futuhi huficha ukali wa masuto kadri inavyoendelea kutuburudisha. Futuhi hulenge kurekebisha tabia inazozidhihaki au inazozichekesha.

### 2.1.2 Maandiko Yahusuyo Ufutuhi

Miongoni mwa waandishi walioandika kuhusu suala la matumizi ya ufutuhi katika za fasihi ni Senkoro (1982:30). Alitumia msamiati wa ucheshi, na kusema:

Ucheshi ni mbinu ya kifani ambayo wasanii huitumia katika kazi zao za fasihi kuzichekesha hadhira zao, au walau kuzifanya hadhira hizo zitabasamu… Wengine hutumia ucheshi ili kuwafurahisha wasomaji, wasikilizaji au watazamaji wa kazi zao; na wengine wanatumia ucheshi ili kuiepushia uchovu hadhira ya kazi zao. Wako paia wasanii ambao hutumia ucheshi ili kujenga kejeli katika kazi zao.

Aidha, amebainisha matumizi mengine ya ucheshi kuwa ni kuundia komedia (futuhi). Pamoja na kwamba maelezo haya yanatupatia mwangaza juu ya matumizi ya ufutuhi katika kazi za fasihi, kwa upande mwingine, yanatuachia maswali muhimu kuhusiana na ufutuhi uliomo katika kazi zingine za kifasihi mfano, kwamba je, tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa mifupa* kwa upande wake zinazo mbinu za ufutuhi? Na kama zimo, ni aina ya mbinu ipi ya ufutuhi iliyotumika kwasilisha suala la elimu juu ya ugonjwa wa ukimwi?

Kezilahabi, (1976), amegusia dhana ya ufutuhi kupitia kipengele cha ubeuzi. Alieleza ubeuzi kwa maana ya kumtania au kumchezea mtu( kwa kufanya dhihaka). Alijenga hoja zake kupitia riwaya za *Kusadikika* (1948) na *Kufikirika* (1946) alibainisha kuwa Shaaban Robert ni mwandishi aliyebobea katika matumizi ya mbinu ya ubeuzi kufikisha maudhui kama vile utu,amani n.k. Katika kubainisha tofauti kati ya ubeuzi na vichekesho anasema: Katika ubeuzi ukweli wake unauma na kuamsha hasira. Katika vichekesho ukweli wake hauumi sana. Ubeuzi unahitaji muda wa kufikiri kwa mtu ambaye kichwa chake ni kizito… Katika vichekesho tunacheka ghafula na katika ubeuzi tunafikiri na kucheka baadaye.

Knapper, (1970) katika kazi yake ya *Myths and Legends of the Swahili,* ameonesha kwamba suala la ufutuhi lilijitokeza hata katika kazi za mwanzo za fasihi ya Kiswahili. Ufutuhi huo ulijikita katika hadithi fupi na mashairi yaliyojaa kejeli na mafumbo baina ya jamii moja na nyingine. Ufutuhi huo haukukusudia kuishia katika kuchekesha tu, bali pia ulitoa mafundisho fulani. Mathalani, anaonesha kuwa Mr Clever man and Mr simple ni miongoni mwa hadithi fupi maarufu za wakati huo.

Kiini cha hadithi hiyo kipo katika msigano baina ya ujanja wa Mr. Cleverman na uzubavu wa Mr. Simple katika kutongoza wanawake. Mr. Cleverman anamfundisha Mr. Simple mbinu mbali mbali za kuwapata wanawake. Baadaya Mr. Simple anafuzu kukubuhu katika hilo. Hatimaye anazitumia mbinu hizo kumpata kimapenzi mke wa Mr.Cleverman mwenyewe. Mr.Cleverman anaanza ugomvi dhidi ya Mr.Simple baada ya kubaini uhusiano huo.

Kazi hii inatupatia mwanga juu ya mambo kwamba, ufutuhi umo katika fasihi simulizi. Pili ufutuhi hutumia mbinu za kukejeli wenye lengo la kutoa ujumbe fulani kwa jamii na tatu ni kwamba ufutuhi huwa na utani ndani yake. Kwa mfano Mr Cleverman alikuwa akimtania Mr Simple kwa uzoba wake wa kushindwa kutongoza wanawake na alipofunzika vizuri alimtongoza mke wa Mr Cleverman na hivyo kuwepo ungomvi tena kati yao. Jambo hilo linachekesha.

Nanjekho,(1998) alishughulikia suala la fani katika tamthiliya za Emmanuel mbogo. Katika tasnifu yake, amezungumzia umuhimu wa wasomaji kuvitambua vipengele mbalimbali vya kazi ya fasihi utambuzi huo hujumuisha pia uhusishaji wa mambo mbalimbali kama vile mazingira na wakati wa utunzi wa kazi husika pamoja na maisha ya mtunzi kwa jumla. Kwa kufanya hivyo msomaji atakuwa katika nafasi nzuri ya kuyafikia malengo na maana alizozikusudia fanani kwa hadhira yake. Kazi hii ilitusaidia sana na kutusukuma zaidi katika azima yetu ya kuchunguza mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dod*o na *Ushuhuda wa mifupa*. Pia ilitusaidia kupata mwanga juu ya asili sifa na maendeleo ya futuhi toka kizazi cha wayunani hadi kuenea kwake duniani kote kupitia mwangaza tuliopata katika kazi hii tukaweza

kuipanulia wigo dhana ya futuhi hadi kupata ufutuhi. Naye Gurdjieff (2008) amefafanua dhana ya ucheshi kwa kutumia mkabala wa kibayolojia. Anabainisha kuwa kicheko ni mwitikio utokeao baada ya mtu kupata kichokoo fulani. Kwa kawaida kicheko hujitokeza kikitanguliwa na tabasabu, kicheko cha sauti huchukuliwa kwa ithibati tu ya nje kuwa mtu amefurahi. Kwa wastani mtu mzima hucheka mara huchukuliwa kwa ithibati tu ya nje kuwa mtu amefurahi. Kwa wastani mtu mzima hucheka mara kumi na saba kwa siku, hivyo maisha ya binadamu yamefungamana sana na ucheshi au futuhi. Kitendo hicho cha mwitiko huzaa furaha ya nanma. Mtu anapocheka hutoa sehemu kubwa ya nishati itengenezwayo na michakato mbali mbali ya mwili. Michakato hii husongana mwilini na kutegeneza sumu inayoweza kudhuru mwili kwa namna mbali mbali.

Gurdjieff (2008) anaendelea kusema sumu hiyo hupunguzwa mwilini kupitia vitendo vya kucheka na kupiga miayo. Mtu huweza kuwa na furaha lakini asicheke na mwingine huweza kucheka hata kama hana furaha, maelezo haya yanahalisi kuwa sio lazima furaha idhihirishwe na kicheko, miguno, tabasamu na ishara nyingine za kimwili kudhihirisha furaha.

Songoyi,(2005) ameshughulikia suala la miundo na maudhui ya nyimbo za Wasukuma. Katika kazi yake, amedhihirisha kuwepo kwa ufutuhi katika fasihi simulizi ya Wasukuma kama ilivyo katika fasihi simulizi za makabila mengine mengi ya Tanzania. Amebainisha aina za utani baina ya makundi ya wasukuma ambapo anatuambia kuwa kuna tofauti kubwa kati ya utani wa vijana na ule wa wazee. Kigezo kikubwa cha tofauti hiyo ni matumizi ya lugha tu utani wa vijana

hutumia lugha kali na ya wazi wakati ule wa watu wazima hutumia tasifida. Amefafanua kuwa utani huo huweza kutolewa kwa kutumia semi simulizi au nyimbo na aina zote hizo za utani hutengeneza ucheshi . Kazi hii pia ilikuwa ithibati angavu kwetu kuhusu kuwepo kwa utangamano wa dhahiri baina ya fasihi simulizi na ufutuhi.

Kazi hii ya Songoyi na mapitio ya kazi tangulizi, zimetusaidia katika utafiti wetu wetu huu kujua aina mbalimbali za ufutuhi ambazo ni pamoja na kejeli, dhihaka,ubeuzi na utani, kwani hili ni moja ya lengo mahususi katika utafiti wetu.

### 2.1.3 Dhima ya Futuhi

Mbogo,(2015). Nukuu za darasani, anaeleza kuwa, Futuhi husababisha mawasiliano ya kisanii kati ya makundi mawili ya watu- waigizaji na watazamaji. Lakini vile vile, futuhi huweza; Hukuza uwezo wa kufikiri na ubunifu wa kisanii kwa watunzi na watazamaji. Mtunzi anapokuwa akipangilia mawazo ili yaendane na mazunguzo na matendo yaweze kuigizwa. Ni chanzo cha ajira kwa vijana hata na wazee kuweza kuwa waigizaji na watunzi wa tamthiliya. Waigizaji hupata pesa kutokana na kujiajiri katika uigizaji. Futuhi inaweza kumpa mtu mwigizaji na mtunzi umaarufu mkubwa akafahamika ndani ya nchi na hata nje ya nchi. Mfano Emmanuel Mbogo, Penina Mhando, Ebrahim Hussein na wengine ni waandishi maarufu wa tamthiliya za Kiswahili katika nchi zote zinazotumia Kiswahili. Wachekeshaji kama Mzee Majuto, Masanja Mkandamizaji, Joti, Mhogo Mchungu, Kigwedu ni watu maarufu ndani ya nchi na nje ya nchi. Futuhi ni chanzo cha maarifa inaweza kutumika katika kuelimisha jamii katika masuala mbalimbali. Kwani kupitia kusoma na kutazama

michezo mbalimbali ya kuigiza watu hupata maarifa mengi. Hii ni pamoja na kuonya, kuadabisha na kuelekeza maadili mbali mbali ambayo yanapatikana katika tamthiliya husika. Futuhi inayo nafasi ya pekee ya kuhifadhi na kukuza utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano majigambo, utani, matambiko, ngoma, harusi, miviga, utambaji wa hadithi na vingine vingi. Futuhi inaweza kutumika kama sehemu ya kupunguza msongo wa kimawazo kwa watazamaji na wasomaji wa kazi ya futuhi kwani huweza kuwafanya wahusika kufurahi, kucheka na hata kusahau matatizo mbalimbali ambayo yalikuwa yanawakabili kabla kutazama futuhi.

Senyabanza,(h.t:77) anasema; “Lengo la msingi la futuhi ni kuchangamsha na huishia kwa namna ya kufurahisha. Lazima tukumbuke kwamba, kusema futuhi inafurahisha haina maana kuwa dhamira yake haina uzito. Futuhi huweza kuwa na sifa zinazotofautiana, jambo ambalo hutumiwa kama kigezo cha kuainisha aina mbali mbali za ucheshi. Lakini, vyovyote iwavyo, futuhi hujikwepesha na maswala ya kuhuzunisha au kushtua”.

Kwa mujibu wa kazi hii, futuhi ni mchezo wa kuigiza au tamthiliya ambao huyaweka mawazo mbali mbali katika matendo ili yaweze kuigizwa katika mtindo wa kuchekesha au kushangaza ili jamii iweze kupata ujumbe uliokusudiwa. Ikumbukwe pia kwamba katika jamii zetu za Kiafrika, jamii zetu tangu zamani zimekuwa na futuhi katika maeneo au miktadha mbali mbali kutegemeana na tukio husika. Kwa mfano, katika sehemu za matanga au katika msiba jamii zetu zimekuwepo na futuhi yenye utani na kejeli ndani yake, bibi na wajukuu nao hufanya futuhi ya aina yake, katika sehemu za ngoma, majigambo nayo pia yalionyesha

ufutuhi ndani yake. Senkoro (2004) anasema, kejeli, futuhi, ucheshi, kijembe, dhihaka na utani huwapo. Kwa ukweli wa hoja hii unajidhihilisha katika maisha yetu ya kila siku ambapo aghalabu kauli zenye kejeli, dhihaka na vijembe huwafanya watu wasikiapo kupata hali ya kicheko au furaha hata kama anayelengwa atakuwa amechukizwa nazo. Aidha kutokana na mwingiliano mkubwa wa kimaana na kidhima uliopo baina ya vijenzi mbali mbali vya ufutuhi tukiamini kwamba kwayo, dhana nyingine za utani, ubeuzi, kejeli, dhihaka na vijembe zitakuwa zimeshughulikiwa kwa pamoja. Kwa msingi huu tasnifu hii imejaribu kuweka mipaka ya kimaana na mifano ya vijenzi hivyo vya ufutuhi ni hivi vifuatavyo:

**Jedwali Na 2.1: Mbinu za Ufutuhi**

| **Mbinu za Ufutuhi** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Ubeuzi | Kejeli | Utani | Dhihaka | Vijembe |

Senyamanza (h.t)

### 2.1.3.1 Ubeuzi

TUKI (2013:37), wanasema kuwa, ubeuzi ni kushushia hadhi mtu kwa maneno au vitendo; dharau, puuza, tweza, dunisha, beau, nyarafu.

Senyamanza (h.t:89), anaeleza kuwa, hii ni aina ya ucheshi ambao hujengwa katika msingi wa dhihaka na pengine kutweza na kumuumiza mtu. Mzungumzaji anatoa kauli, neno au tamko na wakati mwingine mchoro ambao unaweza kuibua kicheko au ucheshi ambao yeye mwenyewe anaishia kucheka,(Wamitila 2008). Ubeuzi hutumia maneno ambayo humhitaji mtu afikiri kwa kina ili kutambua ujumbe uliomo

(Kezilahabi 1976:82). TUKI (2004) wanasema kuwa ‘ubeuzi ni utwezaji, dharau, udunishaji au upuuzaji ufanywao kwa maneno au matendo’. Ubeuzi huhusisha maneno au matendo yanayodhihaki kwa lengo la kushusha hadhi ya mtu au watu na wakati mwingine ubeuzi hutumia mafumbo ingawa si mazito kama kama yatumiwavyo kwenye vijembe. Msanii anaweza kutumia mbinu hii ya ubeuzi katika kuwapa majina wahusika wake na jinsi alivyowaumba na wasifu wao. Mbinu ya ubeuzi imetumiwa pia na Shaaban Robert katika kazi zake. Aina hii ya wahusika imetumika katika Kusadikika(1948). Mfano wa majina yanayoonesha sifa ya ubeuzi ni bwana Karama (mtuhumiwa wa kesi ya kuanzisha uanasheria), bwana Taadabuni(katibu wa serikali) bwana Fujo (mlinda hazina), bwana Komeni (amiri jeshi).

### 2.1.3.2 Kejeli

Ni maneno au matendo yenye dharau, mzaha au kebehi. Msokile {1993:41} anasema: ‘Kejeli au kinaya au shitihizai hukusudia kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa au kinyume na ukweli ulivyo’. Wafula (2007:47-48) anasisitiza kuhusu kejeli kwa kusema kuwa “…kejeli huweza kushambulia, kuchekesha au kuadilisha. Kejeli inayoshambulia bila kuchekesha ni masimango na maonyo ambayo hayakunyunyiziwa chembe za vichekesho ni mahubiri makavu”. Kwa maeelezo hayo ni wazi kuwa kejeli huaambatana na furaha au kicheko ambacho huwafanya wahusika kufurahia.

### 2.1.3.3 Vijembe

TUKI (2013: 222), wanaeleza kuwa, ni maneno ya mafumbo ya kumsema mtu.

Senyamanza (h.t:90) anaeleza kuwa, Vijembe ni tungo au mafumbo au ya mzunguko yenye kumsema mtu kwa mabaya. Mbinu ya kijembe hutumiwa sana katika maongezi ijapokuwa hutumika pia katika maandishi. Sanaa hii hutumia sifa za sitiari kwa kiasi kikubwa{Gibbe,1994; Msokile,1993 na Wamitila,2008} Msingi mkubwa wa ufutuhi unaotokana na vijembe ni mafumbo. Ufutuhi hapa hutokea pale mtu anayetaniwa au kumbiwa mara anapokosa jambo la kujibu na kuonekana kama kaaibishwa.

Msingi huo unatupanulia dhana hii na kuiwezesha kubeba ndani yake namna fulani ya kejeli,dhihaka na mafumbo ambayo huweza  kusababisha hali furaha au kicheko kwa anayesoma au anayesikiliza.

**2.1.3.4 Utani**

TUKI (2013:614), wanaeleza kuwa, utani ni maneno ya kutania, dhihaka, masihara. Vile vile, Ni uhusiano wa wanajamii kuambizana ukweli pasipo chuki kwa njia ya mzaha au dhihaka na zaidi utani hulenga kuchekesha au kufurahisha jamii. Senyamanza, (h.t:91) anasema; Huu ni uhusiano wa kijamii unaoruhusu watu kufanyiana dhihaka na kejeli. Aghalabu, utani hulenga kufurahisha na kuchekesha. Utani unaweza kujitokeza katika umbo la nyimbo, matendo, michoro au hadithi fupi fupi. Kwa ujumla katika jamii zetu za kiafrika utani upo. Kwa mfano katika jamii yetu ya Kitanzania kuna utani kati ya kabila na kabila, kati ya babu na wajukuu na kati ya shemeji mtu na shemeji zake. Kwa upande wa makabila Wasukuma hutaniana na Wazigua, Wapogolo, Wanyakyusa. Wajaruo hutaniana na Wahaya.

### 2.1.3.5 Dhihaka

Muhando na Balisidya (1976:85), anaeleza kuwa ‘Dhihaka ni maelezo au masimulizi yaliyokusudiwa kubeuwa au kudhihaki jambo kisirisiri’.

TUKI (2013), wanaeleza kuwa, maneno au vitendo vya kumfanyia mzaha; tania. cheka, segue. Msokile, (1993:78), anaeleza kuwa, Dhihaka ni maelezo au masimulizi yaliyokusudiwa kubeua jambo kisirisiri. Ni maelezo yanayomdunisha mtu kifumbo. Senyamanza, anaeleza kuwa, Ni maneno au vitendo vya kumfanyia mtu mzaha,utani au masihara.. Wamitila,(2008:396) anasema kuwa; dhihaka ni aina ya kinaya au kejeli ambayo uwezo wake mkubwa hujitokeza katika nguvu za kibalagha. Hii ni aina ya usanii ambayo maneno yanayotamkwa wakati mwingine huandikwa yakizigusa hisia za mlengwa au walengwa kwa namna ambayo inaweza kukasirisha au kuwafanya watizame hali Fulani kwa undani na tafakuri zaidi na mara nyingi dhihaka humfanya mlengwa ahisi ubaya Fulani.

### 2.1.4 Futuhi wakati wa Ukoloni

Muhando na Balisidya (1976:21-28), anaeleza kuwa, baada ya kuja kwa kwa Wazungu kabla ya miaka ya 1960 hapa nchini walituletea futuhi za aina mbali mbali. Walitumia zaidi dini ya Ukristo katika kudharau utamaduni wetu. Futuhi kama zile za mtu asiye na dini alionekana kama kichekesho katika jamii, mtu asiyeweza kuongea lugha ya Kiingereza alionekana kama mshamba na usomi wake kama unao walakini fulani. Kasumba hii imeendelea mpaka leo, wakati mtu akiongea lugha ya Kiingereza huonekana msomi zaidi kuliko Yule asiyeweza kuongea lugha hiyo ya Kikoloni. Mchango wa futuhi tunauona zaidi wakati wa Wazungu katika

mashule ya sekondari,msingi(British council), makanisani na hata katika kumbi mbali mbali za starehe(Little theater). Kisha baadaye katika redio mfano (RTD). Dhamira kuu ya futuhi katika kipindi hiki ilikuwa kuonesha ujinga wa utamaduni wa Mwafrika na kutukuza utamaduni wa Kizungu. Mfano wa kazi zenye ufutuhi zinazoweza kuthibitisha hilo ni;Mshamba wa kioo, Mshamba wa simu, Mshamba wa mji, Mshamba wa mkate na siagi na ile ya Mshamba wa godoro. Kazi zote hizo zilimwonesha Mwafrika kuwa yeye si kitu na Mzungu ni kitu. Hali hii imeathari Sanaa ya futuhi katika jamii ya leo kwani watu waliichukulia Sanaa kama uchekeshaji usiokuwa na maana yoyote ile katika jamii. Kwani hata katika uigizaji wa kawaida,sehemu mbaya huigiza mtu mweusi na sehemu nzuri yenye kutoa mafundisho huigiza mtu mweupe.

### 2.1.5 Futuhi Wakati Ww Sasa Nchini Tanzania

Muhando na Balisidya (1976:28:43), aneleza kuwa, Katika kipindi cha sasa, changamoto mbali mbali zimepungua,kwani sasa kazi ya futuhi inaonekana ya maana katika jamii zetu. Watu, vijana mashuleni,mtaani, redioni, magazetini na kwenye televisheni kipindi cha futuhi kimeonekana kupendwa zaidi na wanajamii. Mfano futuhi inayooneshwa na televisheni ya Star TV,ITV,TBC, televishen ya Chaneli Ten na zingine; waigizaji kama Joti, Mashanja mkandamizaji, Mzee Mjuto, Kigwendu,Bambo na wengine, sasa ni watu maarufu zaidi nchini Tanzania. Kipindi cha futuhi hutazamwa katika familia,kumbi za starehe, kwenye mkesha, simu za mkononi na kwenye vyombo vya usafiri. Tumeshuhudia sehemu za makanisani, misibani na hata katika kipindi cha kampeni za uchaguzi wa Urais, Wabunge na Madiwani wasanii mbali mbali wametumika katika kuhamasisha watu kufika katika

sehemu za kampeni. Msanii kama 'Kigwendu Gwendulile' kwenda kugombea Ubunge katika jimbo la Kisarawe, na kushika nafasi ya pili kwa ushindi! Hii ni hatua kubwa katika nchi yetu si ya kuidharau.Hiyo ni hatua nzuri na katika miaka ijayo fuhuhi itatawala zaidi katika jamii yetu kwani mara zote binadamu huhitaji furaha na sio huzuni.

## 2.2 Pengo la Maarifa

Pamoja na kuwa kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu ulinganishaji wa kazi za tamthiliya, lakini ulinganishaji huo japo ulizingatia masuala ya kimaudhui, lakini si kazi mbili za ufutuhi kuwasilisha ujumbe wa Ukimwi. Vile vile tafiti nyingi zimejikita katika kulinganisha fani na maudhui ya kazi za fasihi, hivyo,bado inaonesha kuwa utafiti wa kina unahitajika ili kutafiti kwa kina jinsi mbinu ya ufutuhi zinavyoweza kutumika kuelimisha jamii kupitia masuala mbalimbali yanayoikabili jamii ukiwemo ugonjwa wa ukimwi na vinavyoweza kumtofautisha na kumlinganisha msanii mmoja na mwingine, katika kazi zao mbili zenye mbinu tofauti za ufutuhi, pengo hili ndilo ambalo utafiti huu umekusudia kuliziba. Ili kufikia lengo hilo, utafiti huu basi, umejaribu kuziba pengo hilo kwa kubainisha Ufuthihi katika tamthiliya za *Embe dodo* na *Ushuhuda wa mifupa*.

## 2.3 Kiunzi cha Nadharia

Ili mtafiti aweze kufanikiwa katika kufanya utafiti, ni lazima awe na nadharia ya kumwongoza ili aweze kujua, anapaswa kufanya nini na mahali gani na kwa kufuata vigezo gani? Mtafiti ataangalia kwa kina nadharia ya fasihi kwani zitamsaidia mtafiti kuchambua data alizonazo kwa kutumia mwanga huo. Nadharia hiyo

itamsaidia mtafiti kujadili kwa unagaubaga nyenzo muhimu katika utafiti wa kutathiminiwa mbinu za kifutuhi katika kuelimisha jamii kuhusu janga la Ukimwi katika tamthiliya ya *Embe Dodo* na *Ushuhuda wa mifupa*.

### 2.3.1 Dhana ya Nadharia

Wamitila (2010:1) anaeleza kuwa, Nadharia ni maarifa ya kitaaluma ambayo msomaji au mhakiki anapaswa kuyajua na kuyafahamu kabla ya kuanza kazi yake. Haya ni maarifa ambayo inatupasa kuwa nayo kabla ya kujihusisha na kazi ya uhakiki. Ni maarifa ambayo yatamwezesha msomaji pia kuyaelewa mambo muhimu, na kwa nja hiyo kuuboresha usomaji wake na uwezo wake wa kufurahia fasihi. Nae, Jilala (2016:59) anaeleza kuwa, nadharia ni wazo ambalo huibuliwa kama mwongozo kwa msomaji ama mchambuzi na hata mwanafasihi linganishi katika kutoa majumuisho ya kazi za fasihi na zisizo za fasihi. Aidha, ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo wa mtu au watu au jamii ya mahali fulani wakati fulani kwa lengo maalumu. Kutokana na maelezo ya Wamitila na Jilala juu ya nadharia tunapata wazo kuwa, nadharia ni ujuzi na utaratibu wenye kanuni maalumu katika wakati maalumu ambao hutumiwa na mwanafasihi linganishi ili kuweza kuhakiki matini husika na kutoa matokeo yaliyokusudiwa kwa mujibu wa nadharia husika.

Wafula na Njogu (2007:2) wanaeleza kuwa, Nadharia ni jumla ya maelekezo yanayomsaidia msomaji au mhakiki kuifahamu kazi ya fasihi kwa kufuata utaratibu maalumu. Nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kuelekeza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani. Mdee na wenzake,wakinukuliwa na Fadhili (2014) wanaeleza kuwa, kwa mawazo hayo nadharia hubeba mawazo, dhana au maelezo

yanayotolewa kwa nia au kwa lengo la kueleza hali fulani, chanzo, muundo utendaji na mwingiliano wa jambo fulani kwa kawaida na kwa kina zaidi.

TUKI (2004) wanaeleza kuwa, Nadharia ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua au kuelekeza jambo fulani. Tunanakubaliana na maana iliyotolewa na TUKI, kutokana na fasili yao imetaja mambo muhimu kama vile maelekezo, mawazo na mwongozo ambao utamwongoza na kumsaidia mhakiki ili kutatua tatizofulani. Katika utafiti wetu dhana ya nadharia imetuongoza katika kupangilia na ubainishaji wa vipengele vya mchomozo. Vilevile imetusaidia kutokwenda nje ya malengo mahususi ya utafiti wetu.

Nadharia ni nyenzo,mawazo maelezo au mwongozo mkuu uliopangwa ili kusaidia kueleza, kutatua na kuelekeza jambo fulani, Kiiango na wenzake (2006) Wamitila (2002), Sengo (2009) . Nadharia ni maelezo kuntu juu ya vipengele muhimu vya fasihi simulizi vinavyopaswa kuzingatiwa na mwanafasihi wakati wa kuhakiki , kuandika, au kutafiti kazi za fasihi simulizi. Kwa mujibu wana mtandao wa wakipedia mwandishi anasema, Nadharia ni mwavuli wa mtalaaluma katika kukabili,kusikiliza, kusoma au kuandika makara mbalimbali za fasihi kwa kuzingatia njia mbalimbali za kifilosofia jinsi mtu anavyotafsiri maana za dhana mbalimbali

## 2.4 Nadharia ya Fasihi Linganishi

Guyard (1964) anasema kuwa fasihi linganishi ni tawi la historia ya fasihi ambapo anadai ni somo la mahusiano, mapatano, na maelewano ya kimataifa baina ya kazi na

maisha ya waandishi wanaotoka katika fasihi tofauti. Wellek (1988) anaifasili fasihi linganishi kuwa ni somo linalojishughulisha na uhusiano wa vitu viwili ambapo vinaweza kuwa kazi ya mtu binafsi, waandishi au kundi la waandishi na binadamu au fasihi kwa ujumla. Kwa upande wake, Wellek (1988) anaiona fasihi linganishi kuwa ni somo la fasihi nje ya mipaka ya nchi moja, ni kujifunza uhusiano baina ya fasihi kwa upande mmoja na eneo lingine la maarifa mfano sanaa, falsafa, historia ya sanaa za jamii, sayansi, dini na mambo mbalimbali ya kijamii. Wellek na Warren (1996) wanaielezea fasihi linganishi kuwa ni mbinu itumiwayo na wahakiki wengi wa fasihi hata wanasayansi kujadili njia maalum ya usomaji wa sanaa mbalimbali ulimwenguni. Wanakubaliana kuwa ni taaluma inayoshughulikia tofauti au kufanana kwa fasihi ya makundi mawili au zaidi ya kiisimu, kiutamaduni, kihistoria, kiitikadi, kiuchumi, kijamii na kimataifa, japokuwa fasihi linganishi inatumika kulinganisha kazi za fasihi za lugha tofauti. Mfano, Kijerumani, Kichina, Kiingereza, Kiswahili na nyinginezo, lakini bado inajishughulisha na fasihi ya lugha moja ikiwa kazi hizo asili yake ni nchi tofauti au utamaduni na vipindi tofauti ndani ya lugha hiyo. Wamitila (2003) anaeleza kuwa fasihi linganishi inahusu uchambuzi wa maandishi ya wakati mmoja na aina moja na katika lugha mbali mbali kwa nia ya kumiliki sifa zinazoyahusisha kama athari, vyanzo, sifa zinazofanana ama kutofautiana za kiutamaduni. Jilala (2016:12-13), anatukumbusha kwamba; "fasihi linganishi ni tofauti na fasihi kwasababu zote ni taaluma zenye kutumia nadharia na mbinu tofauti katika uwasilishaji na matumizi yake". Pia fasihi linganishi ni taaluma inayojitegemea, yenye nadharia zake na ambazo ndiyo msingi wa maarifa ya utendaji wake. Fasihi linganishi katika utafiti huu umetusaidia kuweza kuweka mipaka ya kiulinganishi na pia kujua taaluma ya fasihi linganishi ambayo ndiyo hasa utafiti huu

umekusudia kufanya. Pia fasihi linganishi imetusaidia kujua ni namna gani tunaweza kufanya ulinganishaji wa kazi za fasihi na vipengele vipi vya kuzingatia katika ulinganishaji wa kazi za fasihi katika jamii yetu. Jilala (2016) anasema kuwa, fasihi linganishi inatusaidia kubainisha, kutofautisha, kufanana na kuhusiana kwa fasihi za ulimwenguni, itikadi na mielekeo ya jamii tofauti. Kwa mfano, kwa kutumia fasihi linganishi tunaweza kubaini tofauti za kiutamaduni na kifalsafa za jamii ya Kiswahili. Hivyo katika kazi ya utafiti huu linganishi, utatusaidia kulinganisha na kutofautisha mbinu za Ufutuhi zilizotumika katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuwa wa Mifupa*, katika ubainishaji wa maambuzi na kuenea kwa ugonjwa wa Ukimwi. Katika utafiti na uchunguzi wa kazi za fasihi, zipo nadharia mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kuchunguza na kuchambua kazi za fasihi. Aidha, ni dhahiri kuwa, kila nadharia inaweza kufaa ama kutofaa kuzichambua kazi za fasihi kwa kuzingatia lengo la utafiti. Nadharia nyingine ni Elimu mitindo.

## 2.5 Nadharia ya Elimu Mitindo

Nadharia ya Elimu mitindo katika Uchambuzi wa Matini *(Theory of Stylistics)* ilianzishwa na kutumiwa na Jakobson (1960) na Murry (1976). Tunapojishughulisha na uchambuzi wowote wa lugha ya fasihi, jambo la kwanza analokabiliana nalo mtafiti wa maandishi ya aina hiyo ni mtindo kwa upande mmoja na kwa upande mwingine ni elimumitindo katika nadharia ya sanaa ya lugha. Kihistoria, taaluma ya uchambuzi wa mtindo ilianzia katika kipindi cha karne ya 5 huko Ugiriki na Urumi kabla ya kuzaliwa kwa Masihi. Katika kipindi hiki, balagha au elimu ya usemaji inayohusu ufasaha wa kusema ilikuwa maarufu sana. Taaluma hii ilijumuisha seti za kanuni na mbinu zilizowawezesha wagambi au walumbi na wahutubu (watoaji wa

hotuba maalumu) kuzungumza vizuri kwa kutumia lugha iliyopambwa kwa tamathali za semi na taswira kwa lengo la kuleta mabadiliko katika maoni na fikra za hadhira. Katika nadharia hii, ufundi wa kusema na kuchambua maneno katika kilongo ni njia mwafaka ya kukuwezesha kuwashawishi hadhira wanaokusikiliza ukiwa jukwaani, kanisani au katika kampeni kama za kisiasa. Kwa kuwa njia hii ilikusudiwa kuwaridhisha au kuwaathiri watu wengine kimaono, tukio la kiisimu lenye sura hiyo lilipata umuhimu wa kiulumbi na bila shaka lilichukuliwa kuwa ni ulumbi wa kielimumitindo.

Jilala, (2016:127), anaeleza kuwa, Elimu –mitindo ni taaluma inayoshughulikia mtindo. Ni taaluma ya mitindo mbalimbali ambayo inajitokeza katika mazungumzo, ama maongezi fulani au maandishi ya matini fulani. Ujitokezaji wa ufanano wa aina fulani wa muundo, dhana ya kizungumzwa, kitamkwa, ama matini ni mambo ambayo yanashughulikiwa na nadharia ya elimu-mitindo.

Kwa maneno mengine, lugha ya fasihi iliangaliwa kuwa ilitumia ujumi katika kueneza fikra au ujumbe, ujumi huu ulidhihirishwa katika matumizi ya lugha kisanaa kwa lengo la kuumba wazo na kulisambaza kwa hadhira kwa namna ivutiayo kupita upeo wa matumizi ya lugha ya kawaida. Kwa hiyo, wachambuzi wa kazi za fasihi waliofuata mwelekeo wa Nadharia ya Elimu mitindo katika uchambuzi wa Matini walielekeza jitihada zao za kifasihi katika vipengele kama vile aina ya lugha iliyotumika, taswira, sitiari na picha kwa lengo la kuchunguza jinsi vipengele hivi vilivyotumika kulipamba au kulirembesha jambo fulani kama lilivyowasilishwa katika kazi ya fasihi inayohusika, hivyo umuhimu ulielekezwa katika uteuzi na

upangiliaji wa kisanaa wa maneno katika kazi ya fasihi, huu ni uendelezaji na ukuzaji wa imani kuwa matumizi maalumu ya lugha ni vazi la wazo au fikra. Nadharia inayozingatia mfumo linganifu katika uchambuzi wa matini za kifasihi haikubaliki kwa mujibu wa nadharia ya Elimumitindo *katika Uchambuzi wa Matini*. Hivyo, si sahihi kusema kuwa ubadilishaji wa aina yoyote wa mtindo wa kazi ya fasihi utaleta dosari katika kazi hiyo. Wafuasi wa Nadharia ya Elimumitindo katika Uchambuzi wa Matini wanaamini kuwa kuna mitindo mbalimbali ya kuwasilisha wazo hilo hilo na kwa hiyo katika kazi ya fasihi maudhui na fani ni vitu viwili tofauti. Nadharia hii imetumika kuchambua lengo la kwanza ambalo ni kubainisha mbinu za ufutuhi katika tamthiliya teule. Sababu za kuteua Nadharia hii zimetokana na uwezo wa Nadharia na muhimili wa mawazo ya nadharia hii kuwa itaweza kutuongoza katika kuchambua aina mbalimbali za ufutuhi hatimaye kutuwezesha kuibua dhima mbalimbali za kifutuhi katika tamthiliya teule. Tumeamua kutumia nadharia hii pia kwa kuzingatia kuwa kila mtunzi wa kazi za fasihi huwa na upekee wake unaoweza kumtofautisha na watunzi wengine hata kama wataandika utanzu mmoja na katika kipindi kimoja. Nadharia hii itafaa kubainisha upekee wa kimtindo baina ya watunzi wa kazi zilizoshughulikiwa katika utafiti linganishi.

## 2.6 **Hitimisho**

Sura hii imejadili kazi tangulizi kuhusiana na mambo kadhaa ya kifasihi, kama vile kazi tangulizi zenye kuhusiana na mada yetu ya futuhi,Nadharia ya Elimu mitindo na Fasihi Linganishi ambazo ndizo zimetumika katika utafiti huu, kiunzi cha Nadharia, ambapo mtafiti alichagua kazi tangulizi na tafiti ambazo zina mwelekeo wa kifani, ambapo matokeo ya tafiti zao yametusaidia kutokurudia mada ambayo

tayari imeshataifitiwa. Kutokana na matokeo yao tumegundua kwamba bado upo umuhimu mkubwa wa kufanya tafiti juu ya kipengele cha futuhi, pengo la maarifa na hatimaye, tumepata maarifa mapya ambayo ni ufutuhi na aina zake ambazo ni dhihaka, kejeli,ubeuzi, utani na vijembe. Sura inayofuata ni sura ya tatu, inahusu mbinu za utafiti, katika sura hii mtafiti atabainisha mipaka na mbinu ambazo ametumia katika utafiti huu.

# SURA YA TATU

# 3.0 MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mkabala wa utafiti, mbinu za utafiti zilizotumika ni usomaji wa maktabani na usomaji wa matini, na vifaa ambavyo vilitumika katika utafiti huu. Eneo la utafiti lililotumika ni mkoa wa Dar es Salaam ambao unavyo vyuo vikuu vya kutosha, umewezesha kupata data za kutosha katika utafiti huu. Hivyo, sura hii inajadili kuhusu mbinu za utafiti na hatua zitakazotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu.

## 3.2 Mkabala wa Utafiti

Utafiti huu umetumia mkabala wa kitakwimu na usio wa kitakwimu katika kuzichambua data za utafiti huu. Kama wanavyoeleza (Kombo na Tromp, 2006) kuwa, utafiti wa kitakwimu na usio wa kitakwimu hujazilizana na kukamilishana. Kwa maana hiyo, utafiti huu utahusisha maelezo ya data na pia utatumia nduni za utafiti wa kitakwimu kama vile; matumizi ya namba na asilimia kuelezea matokeo ya data za uchambuzi.

## 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika eneo la jiji la Dar es Salaam, ambapo maeneo kadhaa yalichaguliwa na kutumika kulingana na mahitaji ya utafiti huu. Maeneo hayo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kikuu Huria cha Tanzania jijini Dar es Salaam. Sababu za kuchagua maeneo hayo ni kulingana na upatikanaji wa maktaba

za kutosha ambapo upatikanaji wa vitabu vilivyotajirisha utafiti huu ulikuwa rahisi, ambapo Maktaba kuu ya Tanzania hupatikana, maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hupatikana. Aidha, Dar es Salaam ni eneo ambapo wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili hupatikana hususani tamthiliya ya Kiswahili.

### 3.4 Mbinu ya Usomaji wa Maktabani

Mbinu ya usomaji wa maktabani huhusisha kutafuta data kwa kusoma vitabu mbalimbali kama vile vitabu teule, tahakiki, majarida, na vitabu vya ziada kulingana na malengo ya utafiti, tumeweza kupata data ambazo zimekidhi haja ya kiutafiti. Mbinu hii imetumika katika utafiti huu ambapo mtafiti amesoma na kuchambua vitabu vya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*, pamoja na vitabu vingine vya ziada ambavyo vimewezesha kupata taarifa muhimu katika utafiti huu. Kwa kusoma vitabu mtafiti ameweka bayana mbinu za kifutuhi katika tamthiliya zote na ameweza kugundua namna vinavyotofautiana na kufanana katika utumiaji wa mbinu za kifutuhi. Mbinu hii imefaa sana katika utafiti huu kwani imetusaidia kupata data za kutosha za kiutafiti.

### 3.5 Matini

Vipo vitabu ambavyo vimetumika katika utafiti huu kwa ajili ya kuchunguza na kubainisha mbinu za kifutuhi ambavyo ni *Embe dodo na Ushuhuda wa Mifupa* na vitabu vingine kama vya kiuhakiki ambapo matini hizi zimetusaidia kupata mchango mkubwa katika utafiti huu, kwani data za kifutuhi zimepatikana na kufanikisha utafiti huu.

### 3.6 Uchambuzi wa Data

Data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, ambazo ni uchambuzi linganishi na uchambuzi wa kubainisha, mtafiti amebainisha mbinu za ufutuhi kutoka katika tamthilya teule na kulinganisha utumikaji wa kila mbinu katika kila tamthiliya husika. Pia tukiweka bayana kuwa utafiti huu una sifa za utafiti usio wa kitakwimu na utafiti wa kitakwimu. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu hii kwani inamfaa katika kufikia malengo yake ambapo uchambuzi wa mbinu za kifutuhi umemsaidia kupata mbinu za kifutuhi katika kazi zote mbili za kiusanii na kuona namna mbinu za kifutuhi zulivyotumika katika kuweka bayana njia zinazoeneza ugonjwa wa ukimwi. Uchambuzi linganishi ni mbinu ambayo mtafiti ameitumia katika utafiti huu katika kulinganisha data kutoka katika vyanzo mbalimbali kama kutoka katika matini ya tamthiliya za *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*, ili kupata majumuisho ya namna ambavyo mbinu za kiufutuhi zimetumiwa na wasanii hao. Katika utafiti huu mtafiti amefanya yafuatayo katika uchambuzi wa data:

i) Kubainisha mbinu za kifutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo na Ushuhuda wa Mifupa.*

ii) Kulinganisha na kutofautisha mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*

### 3.7 Hitimisho

Sura hii imejadili juu ya mbinu za utafiti, ambapo eneo la utafiti limebainishwa, Katika ukusanyaji wa data mbinu ya usomaji wa maktaba imetumika kiufanisi na

ndiyo njia pekee ambayo utafiti huu umeitumia . Mtafiti pia ameonesha namna gani mbinu hii ya usomaji makini ilivyo na umuhimu na jinsi ilivyoweza kufanikisha katika uchambuzi wa data kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni uchambuzi mbinu za kifutuhi na uchambuzi linganishi. Sura inayofuata ni sura ya nne, sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

# SURA YA NNE

# 4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne; sehemu ya kwanza inahusu ubainishaji wa mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*, sehemu ya pili**,** inahusu kulinganisha na kulinganua mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*. Na, Sehemu ya mwisho ni hitimisho.

## 4.2 Uteuzi na Matumizi ya Mbinu za Ufutuhi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne: Sehemu ya kwanza ya utafiti huu, mbinu za ufutuhi ambazo zimebainshwa ni pamoja na kejeli, dhihaka, ubeuzi, utani na vijembe. Sehemu ya pili, inahusu kulinganisha na kulinganua kwa mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*. Na, sehemu ya mwisho ni hitimisho.

### 4.2.1 Mbinu za Ufutuhi Katika Tamthiliya ya Embe Dodo

Katika kubainisha mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya Embe dodo na Ushuhuda wa Mifupa, tumebainisha mbinu hizo ambazo ni kejeli, dhihaka, utani, ubeuzi na vijembe.

#### 4.2.1.1 Ubeuzi

Kama tulivyokwisha kueleza kuwa, Ubeuzi huhusisha maneno au matendo yanayodhihaki kwa lengo la kushusha hadhi ya mtu au watu na wakati mwingine ubeuzi hutumia mafumbo ingawa si mazito kama kama yatumiwavyo kwenye vijembe. Ifuaayo ni mifano ya Ubeuzi katika tamthiliya ya *Embe dodo*:uk.1

> *"Wamenitumbulia macho, Nyoooo! Mwembe dodo sio kama mchicha hata katika upandaji wake., Wasilisogelee dodo wanataka walibonyeze, walitepeshe au wakalitoboa walitie kidoda., Hadhira imenyamaza na kumtumbulia macho, Dodo bivu lisilioisha ladha machoni hata kinywani, Asiye na dhambi na awe wa kwanza kumpiga mwanamke kwa mawe"*

Katika sentensi mbalimbali hapo juu, mtunzi amezitumia kwa lengo kushusha hadhi kwa wahusika ili aweze kufikisha maana ya matini aliyoikusudia. Pia, mbinu hiyo imetumika kuonesha mwanamke hakuwa anathaminiwa katika jamii ndiyo maana Bwana Kifaru hakumpeleka mwanae Dodo kwenda shule. Mwandishi anasema;

> *"Wewe ulitaka huyu aende shule kama wewe, hiki chakula angalipika nani?"*

Ubeuzi mwingine umejitokeza pale watu wenye nia mbaya wanapokuwa wakimsifia Dodo ili kumfanya awakubali kwa urahisi. Katika kuthibitisha hili mwandishi anasema; *uk 5*

> *"Harufu yake nzuri puani haibaduki akilini, ukiitoa kichwani itajificha Usimwamshe shetani wangu hata kidogo nakuambia, moyoni na chukua hii mwanangu, ukizidiwa na vishawishi vya waliolemewa na roho ya tama mwovu au … iwe kinga kwako dhiddi ya uchachu ndani ya utamu wa dodo!"*
> Data za utafiti kutoka katika *Embe dodo* (2016)

#### 4.2.1.2 Kejeli

Kama, tulivyokwisha kueleza kuwa, Ni maneno au matendo yenye dharau, mzaha au

kebehi. Kwa maeelezo hayo ni wazi kuwa kejeli huaambatana na furaha au kicheko ambacho huwafanya wahusika kufurahia. Mwandishi wa tamthiliya ya *Embe Dodo* ametumia mbinu hii ya Kejeli ili kufikisha ujumbe wa matini kwa jamii husika. Kwa mfano: *uk 9*

> *"We hayawani, mshenzi, naongea na wewe halafu unaninyamazia na kunian Mimi ni malaika mlinzi wa mti huu hapa kuna dodo bivu linalohitaji ulinzi wa mizimu… Sasa hata kama mimi nikienda itasaidia nini? Inabidi ungojee mpaka mama yenu arudi.undi mtoto? Washenzi wakubwa ningonjeeni hapo hapo niwaonyeshe! Nakwambia lete hapa hiyo nguo, lazima uniambie hili ni gagulo la nani?"*

Mwandishi wa Tamthiliya ya *Embe dodo*, bwana Makukula,ametumia Kejeli hizo hapo kuonesha wanajamii hasa wanaume ambavyo wakati fulani msaada wao ni mdogo juu ya malezi ya mabinti katika jamii yetu.

#### 4.2.1.3 Utani

Kama tulivyokwisha eleza hapo awali kuwa, utani ni uhusiano wa wanajamii kuambizana ukweli pasipo chuki kwa njia ya mdhaha au dhihaka na zaidi utani hulenga kuchekesha au kufurahisha jamii. Ifuatayo ni orodha ya utani uliojitokeza katika tamthiliya ya *Embe dodo*: kwa mfano;*uk 28*

> *"Mimi ni malaika mlinzi wa mti huu hapa kuna dodo bivu linalohitaji ulinzi wa mizimu".*
>
> *Kauli hii imejaa utani wa dharau kwamba Bwana Kifaru hataweza kumlinda binti yake dhidi ya tama za kimwili labda mizimu peke ndiyo inaweza. Kuna kipindi mwandishi ameonesha wanajamii wanaweza kujifanya wako karibu kumbe wao ndiyo waharibifu. Kwa mfano Bwana Maju, mwandishia anasema;*
>
> *" Katu usihofie malezi ya mche dodo wako kwani wewe si mpweke ndugu yangu, jamaa marafiki zako huwa wanakusaidia, aidha kwa samadi au maji ya kumwagilia mche dodo wakati wa kiangazi. Nao mwembe dodo utakua bila shida yoyote"uk1.*

Katika sehemu hii ya Utani kuna kauli zimetumiwa ambazo zinaonesha kama zinachochea wanajamii kufanya ngono zaidi. Kwa mfano, Mama Kifaru anamwambia mwanae Dodo achukue kondomu, jambo hili si jema kwani muhusika anaweza kupitiliza na kufanya kwa makusudi. Mwandishi anasema;uk 6

> BI KIFARU: *Chukua hii mwanangu, ukizidiwa na vishawishi vya waliolemewa na roho ya tamaa mwovu au hata mwema basi na iwe kinga kwako dhidi ya uchachu ndani ya utamu wa dodo!*

Kauli zingine za utani zimetumiwa sehemu mbalimbali, ambazo lengo lake si kufurahisha peke yake bali zimelenga kuielimisha jamii yetu. Mwandishi anasema*;uk 8*

> "*Washenzi wakubwa bahati wamekimbia, Kijani kwa mbali, manjano na rangi ya chungwa inayoangaza., Kutoka chumbani kwa Mwali anatoka mtu mweupe sana anayetoa sauti inayowatisha wote pale subuleni. Mtu anawaka kwa hasira anazungukazunguka na kupigapiga kifua chake akinguruma. Watu wanapomuona Bwana Kifaru na silaha zake wanapiga mayowe wakilia na kukimbia wakitawanyika kila mmoja na njia yake. Mke wa Bw Kifaru na watoto wake wanakimbilia ndani. Manju anakimbia huku akilia kama mtoto mdogo. Mzee amesimama tu, Bw. Kifaru anapomkaribia anampelekea jambia shingoni mzee anagutuka na kulikwepa na kuanguka chini. Manju anasimama na kurudi kumfuata Mzee pale chini alipoanguka. Bw. Kifaru anaendelea kuwatimua wageni wengine. Sio gagulo langu nakwambia leo utasema mwenyewe lake. (Anajitahidi kumzidi nguvu bwana Kifaru) sikubali nasema…*

Mifano hiyo hapo ni mbinu za Utani ambazo zimetumiwa na mwandishi kufikisha ujembe wake alioukusudia katika jamii. Mtu anapokuwa akisoma anaona kama ni ucheshi na utani lakini ndani yake umo ujumbe ambao mtunzi amekusudia uifikie jamii yetu.

#### 4.2.1.4 Dhihaka

Ni maneno au vitendo vya kumfanyia mtu mzaha,utani au masihara. Maneno haya mtu huyasema kwa makusudi ili kumbeza mtu mwingine kisirisiri. Na, kama tulivyokwisha kusema kuwa; dhihaka ni aina ya kinaya au kejeli ambayo uwezo wake mkubwa hujitokeza katika nguvu za kibalagha, Hii ni aina ya usanii ambayo maneno yanayotamkwa wakati mwingine huandikwa yakizigusa hisia za mlengwa au walengwa kwa namna ambayo inaweza kukasirisha au kuwafanya watizame hali fulani kwa undani na tafakuri zaidi na mara nyingi dhihaka humfanya mlengwa ahisi ubaya fulani.

Kwa mfano: Mtu kuitwa "Afisa maembe Dodo" naye anajisikia vizuri kuwa ni Afisa wa maembe dodo, hii dhihaka kubwa ndani yake ambayo imelenga muhusika ajisikie vibaya na kujirudi juu ya tabia mbaya ya Uasherati anayoianya.

Mifano mingine iliyotumika ya mbinu za Dhihaka ni hizi zifuatazo:
" Ajambaye mgoje atakunya tu! Nguo na vitu vingine vya bwana Kifaru vinatupwa sakafuni pale sebuleni. Nguo na vitu vingine vya bwana Kifaru vinatupwa sakafuni pale sebuleni. Kufa shenzi kabisa! Bi. Kifaru anakwenda kwa Afisa na kumpa mkono wake ili afanyiwe uchunguzi. Bi. Kifaru anakwenda kwa Afisa na kumpa mkono wake ili afanyiwe uchunguzi.

Kauli zenye dhihaka zinaonesha hali ya kubeza na kutetea watu wendelee kufanya maovu. Kwa mfano;

> "Dodo lenyewe limeumbwa ili liliwe na watu tunasahau hilo; sidhani kama nafsi ya dodo huridhika linapoiva likaachwa tu

lianuke na kupasuka lenyewe ndipo liokotwe na kuliwa. Hizi ni dhama za mapinduzi. *Tabia* za kila kitu zimebadilika. Hujasikia kuwa vyura wa Kihansi wanazaa kama watu?"

"Katu usihofie malezi ya mche dodo wako kwani wewe si mpweke ndugu yangu, jamaa marafiki zako huwa wanakusaidia, aidha kwa samadi au maji ya kumwagilia mche dodo wakati wa kiangazi. Nao mwembe dodo utakua bila shida yoyote".

MANJU: *Jamani tusiwe wachoyo wa sifa tumshangilie Rabana kwa uumbaji wake mkuu.uk 2*

**4.2.1.5 Vijembe**

Hapo awali tumekwisha kusema kuwa, Msingi mkubwa wa ufutuhi unaotokana na vijembe ni mafumbo. Ufutuhi hapa hutokea pale mtu anayetaniwa au kumbiwa mara anapokosa jambo la kujibu na kuonekana kama kaaibishwa. Msingi huo unatupanulia dhana hii na kuiwezesha kubeba ndani yake namna fulani ya kejeli,dhihaka na mafumbo ambayo huweza kusababisha hali furaha au kicheko kwa anayesoma au anayesikiliza. Mifano mbalimbali imetumiwa na mwandishi ili kufikisha ujumbe kwa njia ya kufumba na kifanya dhihaka au kejeli, lakini lengo la mtunzi si kufurahisha tu. Lengo kubwa ni kufikisha ujumbe wa jamii ijiepushe na njia zinazoeneza Ukimwi. Mwandishi anasema:

*uk 16.*

*" Kwa haraka na papara nyingi anaingia msichana mdogo na kusimama kwa woga akiangalia huku na huko. Mshindi anamwonyesha ishara atulie kimya akifunga mlango. Anapomaliza, Mshindi anamshika msichana mkono na kumvutia chumbani mwake, anamsukumizia ndani anaangalia tena huku na huko, anarudi taaratibu na kuweka ufunguo. Pale mezani taratibu anaingia ndani mwake na kufunga mlango kwa tahadhari kubwa ".*

*"Haya wote sogeeni pale na pangeni mstari mmoja, fanya haraka Sisi tukajipanga. Akaendelea kusema, haya toeni vyote mlivyonavyo na mvitupe mbele yenu". Sisi tukachangamka , mimi*

> *nikatoa kibwera changu cha ugoro na kiberiti changu cha chuma kile ulichoniletea zawadi masika yaliyopita na wengine walitoa vya kwao. Sasa aliyetuhalibia sisi ni yule dereva wetu si alitaka kuzificha zile nauli tulizompatia katika kaptula lake la ndani ohoo pabaya hapo akieleza kwa hisia zaidi. Nakwambia jambazi mmoja alichachamaa, akamnasa kibao cha usoni na kumnyang'anya zile pesa zote "*

Vijembe vyenye dhihaka na kejeli ndani yake pia mifano yake ni hii;

> *"Na hicho kitanda chako ndilo jeneza lako na shuka yako ndiyo sanda yako. Mti huu magamba yake ni nyigu wakali sana bila shaka utakuwa umeanzisha vita na mwishoe utakosa embe dodo. Familia ya washenzi kabisa".*

Hivyo vyote ni vijembe ambavyo mwandishi amevitumia ili kufikisha ujumbe kwa jamii. Kauli kama ya "Dodo haswa, limesheheni mchuzi na nyama" ni kejeli ambayo imelenga kumsifia msichana ili aweze kujiona ni bora zaidi na akubali kwa urahisi kufanya ngono na yule anayemsifia. Hivyo si vyema sana kwa wanajamii kuwa wanawasifu wasichana kumbe ndani yake wamekusudia mambo mabaya. mwandishi amemtumia Manju akimsifia Dodo na matokeo yake ndiye aliyekuja kuwa mpenzi wake.

### 4.2.2 Mbinu za Ufutuhi katika Ushuda wa Mifupa

Utafiti huu ulichunguza mbinu za Ufutuhi katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* na kubaini kuwa mtunzi wa tamthiliya hii ametumia mbinu za Ufutuhi katika uwasilishaji wa maudhui ya kazi yake ametumia mbinu za ufutuhi zenye kufurahisha na kueleweka kwa kuweka wazi maudhui anayoyawasilisha pamoja na ugunduzi huo baadhi ya mbinu za ufutuhi zilizobainika ni kama ifuatavyo:

#### 4.2.2.1 Mbinu za Ufutuhi

Mbinu za ufutuhi zilizobainishwa katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* ni; ubeuzi, utani, kejeli, vijembe na dhihaka. Lengo lilikuwa ni kubaini mbinu ya ufutuhi iliyotumiwa mara nyingi zaidi. Matokeo yalikuwa kama yanavyojionesha kupitia mbinu mbalimbali hapa chini;

#### 4.2.2.2 Vijembe

Bado tunakumbushia kuwa ,Msingi mkubwa wa ufutuhi unaotokana na vijembe ni mafumbo. Ufutuhi hapa hutokea pale mtu anayetaniwa au kumbiwa mara anapokosa jambo la kujibu na kuonekana kama kaaibishwa. Msingi huo unatupanulia dhana hii na kuiwezesha kubeba ndani yake namna fulani ya kejeli,dhihaka na mafumbo ambayo huweza kusababisha hali furaha au kicheko kwa anayesoma au anayesikiliza. Utafiti huu uligundua kuwa msanii wa *Ushuhuda wa Mifupa* ametumia vijembe katika kujenga maudhui ya kazi yake. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya vijembe ambayo ilibainishwa katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa*:

MTU 2: *"Nesi kwani ukipiga hivi hivi tu haziingii?( uk 6)"*

Hiki ni kijembe kwa mtumishi wa idara ya Afya ambapo wagonjwa wanamuuliza na yeye bila ya kuwa makini anakubali na kuanza kuwachoma sindano wagonjwa wake. Mwandishi ametumia kijembe hicho chenye kejeli ndani yake kuwakumbusha raia na serikali kujali Afya za watu. Mfano mwingine ni huu wa Daktari kumchoma mgonjwa sindano koridoni bila hata ya kuzichemsha na anatumia sindani ileile kwa kila mgonjwa. Kwa mfano:

*(Wanachepuka kando) na kuanza kuongea lakini hatusikii. Tunaona tu kuwa anafungua begi lake tena, anapokea fedha na kumdunga sindano.(uk 9).*

MTU 2: *Mtoto mwoga wa sindano huyo. (uk 6) .*
*Lakini waoga watupu Huja yao vya bure tu. Ukiwaona jeshi kidogo wanasahau walivyoagizwa ...( uk 7),*

MTU 4*:* *Na wewe mtani wangu kwa woga! Hivi hapo ulipo unatamani kukimbia hizo sindano.(uk 6)*

MTU 1: *(Akikimbia ) Yalaaa… tumekwisha .(Anaingia na kumfukuza Korido – dokta ) Wewe shetani kabisa Unatangaza Ukimwi hadharani unadhani togwaaofanya Kazi kuzurura tu Ukimwona mtu anavipele kidogo basi ameshakuwa na Ukimwi. (uk 19).*

Vile vile mwandishi ametumia mbinu ya vijembe kuonesha jinsi wanajamii ambavyo hawajui chochote juu ya ugonjwa wa Ukimwi. Mtu anajisifu kufa kwa ugonjwa wa Ukimwi kuwa ni ushujaa, jambo linaloonesha ujinga mkubwa kwa jamii yetu. Kwa mfano:

MTANI*:* *Nzi kufia kwenye kidonda si haramu, acha ushamba.(uk 17),*

MTANI*:* *Na ukimtunza mgonjwa wa ukimwi basi kachimbe kabisa na kaburi lako, usitupe shida sisi watani.(uk 19)*
*Umekwisha ndugu, siwezi kukutibu. Una Ukimwi! (uk 19)*

MTAMBAJI: *Makalikiti na Toza, baada ya kila mteja kuondoka, wanarudi na kujiweka sawa mapambo yao tayari kuwavutia wateja wengine.(uk 11)*

Pia, mwandishi vijembe kuonesha umaskini na tama vimechangia katika kueza ugonjwa wa Ukimwi katika jamii yetu. Mwandishi anasema:

*("Wateja wanapita wanatoa fedha, na kufuatana na Malaya wale pembeni au nyuma")…(uk 11)*

MTU 4: *Mie siku hizi natumia dezeli kwenye kibatari changu (uk 6).*

MTANI*:* *Dezo naye amesika Makalikiti kafa akili zimemduru! A anatapatapa kuzidi kuku anayetaka kutaga .Anataka hata kucholopoa nguo. Jana jioni nimemwona anakwenda mkojo inamporomoka",(uk 16)*

Maelezo ya hapo juu yanawasilisha mifano ya mifano ya mbinu za vijembe ambavyo vimetumika katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* ambapo Msanii ametumia mbinu za vijembe kujenga maudhui mbali mbali ambayo yamejitokeza. Mfano "'Nzi kufia kwenye kidonda si haramu, acha ushamba' anawasilisha maudhui ya ugonjwa wa ukimwi kuwa hauna tiba na mtu akiwa na ugonjwa huo lazima atakufa tu. Aidha ameionya jamii yetu kuepukana na imani potofu kwani ugonjwa wa ukimwi hauambukizwi kwa mtu kula chakula kimoja na mgonjwa wa ukimwi.

**4.2.2.3 Dhihaka**

Katika kuchunguza na kuchambua tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa*, utafiti huu ulibaini kuwa msanii ametumia mbinu ya ufutuhi dhihaka katika kujenga maudhui ya kazi yake. Mifano mbalimbali inadhihirsha kuwa dhihaka zimetumika kisanii kujenga maudhui ya tamthiliya hii, dhihaka imetumika kama mbinu ya kuhamasisha harakati za ukombozi dhidi ya ujinga kwani ujinga ndio unasababisha kuenea kwa ukimwi, kuthamini afya katika jamii, orodha ifuatayo inaonesha mifano ya dhihaka iliyotumika. Kuna dhihaka zilizoja mzaha ndani yake. Kwa mfano:

MUUGUZI: …*"Tena nilichemsha kiasi jana, kabla mafuta hayajaisha kabisa (uk 6).*

DAKTARI: *Sogea huko kwa manesi utoe damu ili tuweze kuokoa maisha ya mwezetu…manesi wanamtoa damu, hapo hapo Daktari anamwekea mgonjwa harafu wanamweka kando.(uk 7)*

MATANI*: Mwishowe nikalazwa hospitali…basi nikawa nasubiri huku nikiomba, siku ya tatu tangu nilazwe, nikaamka na kuona mwanga mkubwa! Nikaambiwa imani yako imekuponya! Na si hivyo tu, umepata uwezo wa kuponya wagonjwa,viwete…wagonjwa wote wengine.(uk 16)*

MTANI: *Ngonjeni kidogo jama msife. Nasikia ndugu zetu wamegundua Kemroni, kiboko ya Ukimwi.(uk 20)*

KORIDO DOKTA*:*

*Loh… Pole sana mwananchi . Ngoja nikuchunguze .Yaa.. Nywele zako zimekuwa nyekundu naona Ah sijui kwanini…(uk 19)*

MTANI*: Ahaaa Nakuona tu kuwa kilio hiki kinakuhusu …Na wewe unumunasaba nao sio Ndugu yao sema upesi tukutoze faini ya kuchelewa kufika….(uk 15) .*

MTU 3: *Safi. Jujuoloji imeonesha kuwa ugonjwa huu umeanzia kwa wafungwa waliokuwa wanabashiana huko Marekani.(uk 5)*

MENEJA DOKOA:

*Nami nitashukuru saana kama lugha zetu zitaelewana kidogo. Usiogope mtoto, tunaweza kwenda. Usiwe na shaka na Meneja-Dokoa.( Wanacheka. Wanashikana mikono na kuondoka pamoja...) (uk 13).*

Mifano mingine ya dhihaka imetumiwa na mwandishi kuonesha wanajamii kutokujali na masihara, mifano ifuatayo inadhihirisha hicho:

MTU 5*: "Ripoti yenyewe bwana, ni kwamba kuna watu wametengeneza hivi viini kwenye lebu…Er…Yaani kwenye maabara. Sijui makusudi au kwa nasibu, viini hivi mwishowe vikatoka huko kwenye maabara, vikasambaa. Vilisambaa toka wapi? Toka kwenye maabara moja huko Marekani.(uk 5).*

MTU 3: *Siye jadi yetu kwenda ngomani. Basi tuache utani, nimekuja hapa kuangalia kama nina kimeo maana nakohoa mno!(uk 10)*
*Hili stovu halina mafuta hata tone. Hizi sindano tutapigaje leo jamani? Hii zahanati yetu nayo imezidi kwa matatizo.(uk 6)*

MUUGUZI: *Unaweza kukumbuka grupu lako?(uk 7)*

MENEJA DOKOA*:*
*No! Tiba ipo! Lazima ipatikane. Mimi ni Waziri-Mdogo. Nitaagiza kondomu bilioni mia mbili! (uk 17)*

MTAMBAJI*: Na si hivyo tuma umepata uwezo wa kuponya Wagongwa, viwete, wako vichaa ,vipofu mababu waliopooza na wagojwa wote wengine Njooni kwangu mpate tiba …(uk 16)*

MTAMBAJI: *Kumbe ana kifua kikuu Unaona basi . Mtu konfyusheni tupu . Mtu akichongeka kwa gongo likamuuma utasema Ukimwi( uk 19)*

Dhihaka nyingine mwandishi amezitumia kubeza tabia zisizofaa katika jamii ambazo zinatumiwa na wanajamii. Mifano yake ni hii ifuatayo:

MTAMBAJI: "Kemroni itaponyesha wengine siyo wewe!... vaa *sanda chimba kaburi lako!(uk 21)*

MAKALIKITI:
*Washenzi wale! Wanadhani sisi tutakula nini wakifunga maduka yetu?(uk 11).*

MTU 2: *Ulishike hilo baba zima (uk 6).*

**4.2.2.3 Utani**

Ni uhusiano wa wanajamii kuambizana ukweli pasipo chuki kwa njia ya mdhaha au dhihaka na zaidi utani hulenga kuchekesha au kufurahisha jamii. Senyamanza (h.t) anasema; Huu ni uhusiano wa kijamii unaoruhusu watu kufanyiana dhihaka na kejeli. Aghalabu, utani hulenga kufurahisha na kuchekesha. Utani unaweza kujitokeza

katika umbo la nyimbo, matendo, michoro au hadithi fupi fupi. Kwa ujumla katika jamii zetu za kiafrika utani upo. Kwa mfano katika jamii yetu ya Kitanzania kuna utani kati ya kabila na kabila, kati ya babu na wajukuu na kati ya shemeji mtu na shemeji zake. Kwa upande wa makabila Wasukuma hutaniana na Wazigua, Wapogolo, Wanyakyusa. Wajaruo hutaniana na Wahaya.

Mwandishi wa tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* bwana Ngozi, ametumia mbinu hii ya utani kuonesha kejeli na dhihaka ili kufikisha ujumbe wa jinsi ungonjwa umavyoenea na jinsi raia tusivyokuwa makini. Mifano ifuatayo inathibitisha hilo:

MTU 2: *“Basi tudunge tu hizo sindano mama, hamna taabu.(uk 6)… Nikaona nipunge upepo kidogo. Unajua tena dereva lazima uwe na spea taya.(uk 8).*

KORIDO DOKTA*:*
*Sindano moja tu itakausha.(uk8).*

NGARIBA: *Funua mdomo ehee! Unacho(anamkata). Ee naona leo mko wengi sana wateja wangu. Hivyo bora mfungue midomo na kuachama.(uk 10).*

MTANI: *Jama hii balaa! Hivi viini hatari, nasikia ukikanyanga tu mavi au matapishi ya mgonjwa wa ukimwi tayari umeshaupata!...Akikupigia chafya tu basi umeshakukumba na wewe... Tena ukimpa mkono tu ndiyo umekwisha…. Ukishirikiana nao wenye Ukimwi vyombo vya chakula,vyoo au vinywaji ndiyo tena umeshanunua sanda!(uk 18)…Yalaa tumekwisha! Wote hakuna cha Bwana Vodka na Doladola, walajujumani, wala Yohana mtembezi, wala nani! Tumekwisha! (uk 20).*

MENEJA DOKOA:
*Na hivi unavyoniona, natoka Sweden, er…tulikuwa na mikutano yetu ya kimataifa.(uk 14).*

MTANI: *Nina uwezo! Nina nguvu!...Nina uwezo…Basi mimi ninakwambia Toza, bwana Toza tumpeleke Makalikiti shoga yako kwa Yule bwana muombaji.(uk 16)*

MTAMBAJI: *Ah! Bwana hata haieleweki vizuri. Lakini nimesikia watani wanapitapita hapa wanasema kuwa amekufa kwa Slimufiti…(uk 15).*

MENEJA DOKOA:
*Oh! Kumbe unanifahamu…er…Ndiyo. Jina langu ni Meneja –Dokoa…lakini siku hizi nimepata uwaziri mdogo kwenye Wizara mpya ya Kondomu. (uk 14).*

MTU 3: *Shenzi mwenyewe…! Nitakuroga nikugeuze fisi mahamri wee!(uk 5).*

MENEJA DOKOA*:*
*Er…nilikuwa naulizia, ugonjwa aliokuwa, akiumwa marehemu Makalikiti.(uk 15).*

MTANI: *Acha Iniue Dogodogo siachi!(uk 15) Jama ajabu hii (Anacheka )*

MTANI: *Tangu Makalikiti amekufa najionea vionjo vinatokea Juzi mabwana watatu. Maji na yao yanahifadhi, watu wenye. Heshima kidogo, waliposikia kuwa Makalikiti amekufa, wameacha kazi na kurudi makwao Ghafla tu .Mh! Vituko haviishi Mzee.(uk 15-16)*

Hiyo ni mifano mbalimbali ambayo imetumiwa na mwandishi akionesha hali halisi ilivyo katika jamii na hali hiyo ndiyo imechangia zaidi katika kueneza ugonjwa wa Ukimwi katika jamii yetu.

#### 4.2.2.4 Kejeli

Kama tulivyokwisha kusema kuwa, Ni maneno au matendo yenye dharau, mdhaha au kebehi. Kwa maeelezo hayo ni wazi kuwa kejeli huaambatana na furaha au kicheko ambacho huwafanya wahusika kufurahia. Katika kuchunguza na kuchambua tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa*, utafiti huu ulibaini kuwa msanii ametumia mbinu ya ufutuhi kejeli katika kujenga maudhui ya kazi yake. Tuangalie mifano

ifuatayo, jinsi invyowasilisha mbinu za kejeli iliyotumika katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa.* Ambayo ni kebehi:

MTANI: *Hakuna mtu wa kumzika mwenzaie! Sote tulitopea mno kwenye uasherati.(uk 20)*

MTU 2: *Nesi kwani ukipiga hivi hivi tu haziingii? (uk 6) . Vizuri sana, maana damu yako anaweza kupewa mgonjwa yeyote.( uk 7).*

DAKTARI: *Asante kwa waziri mdogo wa kondomu jukumu letu ni kubwa, lazima tuzichanagamkie.( uk 18)*

MTU 2: *Utafiti madhubuti wa hali ya juu kabisa huo. Msitutishe na sisi Waafrika tumetazamia. Msinikodolee macho kama vyura. ( uk 5).*

MENEJA DOKOA:

*Mimi naitwa Meneja-Dokoa, Eeer… ni meneja wa kampuni ya Kondomu…Ha! Ha! Ha! Ni mtu mkubwa kidogo. Tunanunua na kuuza kondomu nchi nzima.(uk 12).*

*Kejeli zingine zilizotumika zinaonesha dharau , mzaha na shambuli. Mifano ifuatayo inathibitisha hilo:*

KORIDO DOKTA*:*

*Nimeenda hata ng'ambo kuspeshalizi, nimerudi hapa sipumui kwa kuwahudumia wagonjwa waliorundikana, halafu wananipa mshahara wanaoita wa mwezi. Lakini nakula siku tatu tu, umekwisha! Sasa nitafanyaje? Basi kila mtu Alipoona anashindwa , kuanza AH,huyu ana pepo mbaya huyu. Na huyu mwanamke , unaona macho yake kipofu ( uk 16).*

KORIDO DOKITA:

*Begi hii ina kila kitu… ndivyo tutakavyoishi na sisi. Kila mtu mahali pake. Na mimi mahali pangu kwenye begi hii… Ndiyo hata Kuhani chakula chake anapata hekaluni, ati, hivyo nitaji… (uk 7).*

*(Ngariba anapita akikata vimeo kwa mkasi wake ule ule kwa haraka haraka mno).( uk 10).*

MTU 4: *Wamezoea hawa Wamarekani; kila kitu kibaya, ni cha Mwafrika. Maluuni hawa! Hata huko kwenye mwezi wanakokwenda siku wakikuta mavi watasema sisi*

*ndiyo tuliokunya huko. Mabaradhuli wakubwa! (uk 4).*

MTAMBAJI: *Kumbe ana matetekuanga. katika hali ya utupu. Meneja DOKOA anaanza kumnyemelea.(uk 19).*

MTANI: *Anafyatuka kama risasi!...Nawaambia makubwa! Ugonjwa huu hauna tiba hata ya kuombewa! . (uk 16)*

DAKTARI*: Tumia mpira ni kinga bora! Mabibi na mabwana tumieni mipira! Hii ni kinga bora ya ukimwi. Vaeni hivi(wanavaa wote mipira kwenye vidole).(uk 18).*

MTANI: *Kila mtu avae sanda yake. (uk 20)*
*Ajabu ……Lete Maji tumwagie atainuka (wanaendelea kumuhudumia ) (uk 15).*

TOZA: *Aa, sasa hivi tu, kama tumefuatana tuseme. Hapa naona kama pazuri wale njuga (uk 11)*

**4.2.2.5 Ubeuzi**

Kama tulivyosema kuwa, hii ni aina ya ucheshi ambao hujengwa katika msingi wa dhihaki na pengine kutweza na kumuumiza mtu. Mzungumzaji anatoa kauli, neno au tamko na wakati mwingine mchoro ambao unaweza kuibua kicheko au ucheshi ambao yeye mwenyewe anaishia kucheka. Mfano ya Ubeuzi ifuatayo inaonesha Ubeuzi wa dharau na kudunisha:

MTANI: *Basi akaomba alipoona anashindwa, kaanza " Ah, huyu ana pepo mbaya huyu. Na huyu mwanamke unaona macho yake. Kipofu! Lazima atubie dhambi zake. Na ashukru amekuwa kipofu kwani angekuwa na macho angekuwa muovu zaidi.(uk 16)*

DOKTA KORIDO:
*Wewe umepatikana tena Utakatika hiyo ndude yako. Chunga sana (uk 8).*
*(Anaingia MAKALIKITI akiwa amevaa sketi fupi mno kiasi cha kuyaacha mapaja katika hali ya utupu. Meneja DOKOA anaanza kumnyemelea.(uk 12).*

MTAMBAJI*: Khe! Hata mimi sikujua kwamba Ngariba alikuwa pia mkata vimeo. Salale! Haya tena, mwenye macho haambiwi ona. Ndiyo viini vilivyoenea hivyo. Lakini*

*yote hayo ni upuuzi ukulinganisha na sababu yenyewe hasa iliyosababisha mji wetu kuteketea.(uk 10-11)*

MTAMBAJI: *Meneja –dokoa alizunguka nchi zima kutafuta dawa.katibu maji , kajaribu MM 11 wapi kajaribu Moro kuna mambo , haikufua dafu . Mwishowe akarudishwa hospitalini Kwa wanashinda kutwa nzima kumsafisha nakumpa dripul Lakini wapi anazidi kukonda na kuishiwa nguvu .(uk 20).*

Mfano mingine ya mbinu za Ubeuzi ambazo mwandishi amezitumia ni dhihaka. Tauangalie mifano ifutayo:

MTU 1*:* *Eh mwanangu hata vinaeleweka Mtoto alianza tu kuwa anachokachoka tu kila wakati. Ghafla akawa vijihoma homa havimwishi , mara kuharisha mara kwa mara kutapika.Kutapika ndiyo kutapika mwanangu, dawa na dawa tumemaliza. Waganga nawaganga na wauguzi Wapi Mtoto anazidi kunyangonyea tu. Khe mara tukaanza kumwona anapata utando mweupe mdomoni. Nywele zikaanza kumngoka kichwani.Sisi tukafikilri labda kwaajili ya yale madawa yao yakutengeneza nywele ,maana nasikia huwa yanahalibu nywele mwishoni .(uk 13)*

KORODO DAKTA:
*Ha! Ha! Ha! Utaniona wapi tumo kwenye korido kidogo kidogo (uk 8)*

NGARIBA: *Si vimeo tu. Kutahiri watoto na hata wakubwa ndiyo mwenyewew mimi.(uk 10)*

Kuna ubeuzi wa kuumiza ambao mwandishi ameutumia kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Mifano ifuatayo inathibisha hilo:

MIFUPA: *(wote) Ndiyo, umeupata! Na wewe umeupata! Na mimi nimeupata! Na Yule ameupata! Na Yule na yulee…! Ni wewe umeniambukiza. Ni wewe…Ni wewe…Ni wewe…wewe…(uk 2)*

Ubeuzi mwingine uliotumika kwa lengo la kuibua kicheko. Mfano ufuatao unathitisha hilo:

MENEJA DOKOA:
*Nami nitashukuru saana kama lugha zetu zitaelewana kidogo. Usiogope mtoto, tunaweza kwenda. Usiwe na shaka na Meneja-Dokoa.( Wanacheka. Wanashikana mikono na kuondoka pamoja…) (uk 13)*

Mdafao wa ujitokeza wa vipengele vya mbinu za Ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*.

Utafiti huu ulichunguza mdafao wa ujitokezaji wa mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*. Matokeo yalikuwa kama yafuatayo:

**Jedwali Na 4.1: mbinu za Ufutuhi katika Embe dodo na Ushuhuda wa Mifupa**

| **Mbinu za ufutuhi** | ***Embe dodo*** | ***Ushuhuda wa mifupa*** |
|---|---|---|
| Kejeli | 11 | 19 |
| Ubeuzi | 15 | 10 |
| Vijembe | 08 | 14 |
| Dhihaka | 17 | 18 |
| Utani | 17 | 18 |
| Jumla | 69 | 79 |

Jedwali Namba 4 linawasilisha ujitokezaji wa mbinu za Ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* . Data inadhihirisha kuwa mbinu za zaidi ya za utani na dhihaka katika tamthiliya ya *Embe dodo* ambazo zimejitokeza zaidi kwa mara 17 kila moja. Wakati kwa *Ushuhuda wa Mifupa* mbinu ya kejeli imejitokeza mara 19 zaidi ya mbinu ya dhihaka na utani zimejitokeza mara 18 kila moja. Ukweli huu unajitokeza wakati msomaji anaposoma tamthiliya hii ya *Ushuhuda wa Mifupa* hufurahia sana kutokana na matumizi ya mbinu ya kejeli kuwa kubwa zaidi ya mbinu nyingine kwenye tamthiliya hiyo. Wakati mtunzi wa tamthiliya ya *Embe*

*dodo* ametumia mbinu ya kejeli mara 11. Mbinu nyingine ni ubeuzi iliyotumiwa na msanii wa *Embe dodo* mara 15 na mara 10 katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa mifupa.* Na mbinu ya vijembe imetumika katika *Embe dodo* mara 8 na mara 14 katika *Ushuhuda wa Mifupa*. Mbinu hizo za ufutuhi zinamfanya msomaji kutafakari kwa umakini ili kupata maudhui yaliyokusudiwa na watunzi yafike katika jamii husika na ugumu wa kumfanya msomaji atafute maana halisi ya kazi ya sanaa.

## 4.3 Kulinganua na Kulinganisha Uteuzi wa Mbinu za Ufutuhi Katika Kuwasilisha Ueneaji wa Ukimwi

Utafiti huu ulichambua na kuchunguza mbinu za ufutuhi zilivyotumika katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* ili kuona ni jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizo wanatumia mbinu za ufutuhi katika kuwasilisha maudhui. Je, kuna kufanana ama kutofautiana katika uteuzi wa mbinu za ufutuhi ili kuwasilisha masuala ya ukimwi katika jamii? Matokeo ya utafiti huu yalikuwa kama yanavyowasilishwa katika vipengele vifuatavyo.

### 4.3.1 Kutofautiana

Katika uchunguzi wetu, utafiti huu ulibaini kuwa, wasanii wametumia mbinu za ufutuhi kwa namna tofauti na uteuzi wa mbinu hizo unatofautiana kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano ilibainika kuwa katika *Embe dodo,* msanii ametumia zaidi mbinu ya ufutuhi dhihaka kwa mara 17 na mbinu ya utani kwa mara 17 katika kuielimisha jamii yetu kuhusu janga la ugonjwa wa ukimwi ulivyoenea zaidi katika nchi ya Tanzania katika kipindi cha miaka ya 1980 hadi 2000 na harakati za kupambana na ugonjwa huo. Mfano wa mbinu ya dhihaka zilizotumika ni

> *"Katu usihofie malezi ya mche dodo wako kwani wewe si mpweke ndugu yangu, jamaa marafiki zako huwa wanakusaidia, aidha kwa samadi au maji ya kumwagilia mche dodo wakati wa kiangazi. Nao mwembe dodo utakua bila shida yoyote." Na "Dodo lenyewe limeumbwa ili liliwe na watu tunasahau hilo; sidhani kama nafsi ya dodo huridhika linapoiva likaachwa tu lianuke na kupasuka lenyewe ndipo liokotwe na kuliwa. Hizi ni dhama za mapinduzi. Tabia za kila kitu zimebadilika. Hujasikia kuwa vyura wa Kihansi wanazaa kama watu?".*

Tofauti na tamthiliya ya *Ushuhuda wa mifupa* ambayo mbinu ya dhihaka imetumika kwa mara 18 na utani nao umetumika kwa mara 18. Mfano wa wa dhihaka zilizotumika ni pamoja na

> *"Tena nilichemsha kiasi jana, kabla mafuta hayajaisha kabisa", "Unaweza kukumbuka grupu lako?" na "Sogea huko kwa manesi utoe damu ili tuweze kuokoa maisha ya mwezetu…manesi wanamtoa damu, hapo hapo Daktari anamwekea mgonjwa harafu wanamweka kando".*

Tofauti nyingine ambayo utafiti huu umebainisha ni mbinu ya kejeli iliyotumiwa na msanii wa tamthiliya ya Embe dodo na mifano baadhi iliyotumika ni ;

> *"Toka na marapurapu yako yote hayawani mkubwa!", "Wewe ni kiziwi hunisikii?", "Huwezi kunivua nguo mbele za watu halafu nikuache hapa ndani hata siku moja, leo unarudi kwenu!", "Anaikagua ile pakiti na kuitupa chini" na "Mimi ni malaika mlinzi wa mti huu hapa kuna dodo bivu linalohitaji ulinzi wa mizimu".*

Wakati katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* ambayo imetumia zaidi mbinu ya dhihaka ambayo imejitokeza kwa mara 18, tamthiliya hii imejaa mbinu za kuchekesha kiasi cha kuwafanya wasomaji na wasikiliza wapende sana kuisoma na kuisikiliza tamthiliya hii. Mfano wa kejeli zilizotumika ni pamoja na.

> *"Nesi kwani ukipiga hivi hivi tu haziingii?" na "Vizuri sana, maana damu yako anaweza kupewa mgonjwa yeyote."*

Kejeli ambazo humvutia msomaji kuona jinsi ujinga ndani ya jamii ulivyosabalisha kuenea kwa ugonjwa wa ukimwi. Watu hawajui umuhimu wa kuchemshwa kwa sindano kabla ya kuchemshwa.

### 4.3.2 Kufanana

Kwa mujibu wa Jilala,(2016) katika zile kanuni za ulinganishaji wa fasihi anasema " Mwanafasihi linganishi anapaswa kuzingatia na kuelewa muktadha wa utamaduni wa jamii iliyozaa kazi za fasihi anazozifanyia kazi". Na sisi katika utafiti huu tunazingatia hilo kwani muktadha wa utamaduni uliozaa kazi hizi mbili, *Embe dodo* na *Ushuhuda wa mifupa* ni ukosefu wa uelewa katika jamii yetu juu ya ugonjwa wa ukimwi na maambukizi yake. Kwa mfano katika tamthiliya ya *Embe dodo* mwandishi anatuambia kuwa kitendo cha Bibi Kifaru kumpatia kondomu binti ya Dodo awe anaitumia pindi anapozidiwa na tamaa kilichukuliwa kama ukosefu wa adabu, utovu wa maadili na kumhamasisha binti yake kufanya ngono. Mwandishai anasema:

> *BIBI KIFARU: Chukua hii mwanangu, ukizidiwa na vishawishi vya waliolemewa na roho ya tamaa mwovu au hata mwema basi na iwe kinga kwako dhidi ya uchachu ndani ya utamu wa dodo!*

Jambo hilo halikuwa zuri kwa bwana Kifaru pale alipoamua kumfukuza mke wake kwamba amemuaibisha mbele ya watu na amemhamasisha binti yao kuwa kahaba. Vile vile mwandishi wa *Ushuhuda wa mifupa* ameonesha ukosefu wa elimu juu ya ugonjwa ukimwi ulikuwa mkubwa katika jamii yetu, watu walikuwa hawana elimu sahihi juu ya kuenea kwa ugonjwa huo. Mtunzi anasema;

> *"Jamani hii balaa! Hivi viini hatari, nasikia ukikanyanga tu mavi au matapishi ya mgonjwa wa ukimwi tayari umeshaupata!".*

> *"Akikupigia chafya tu basi umeshakukumba na wewe" na Tena ukimpa mkono tu ndiyo umekwisha…"*

Mfano mwingine anaoutoa mwandishi ni mila na desturi za wakati ule ndizo zilizaa tamthiliya hii ya *Embe dodo*, pale wanajamii wanapoona kuwa mwanamke ameumbwa ili kuwastarehesha wanaume tu. Mwandishi anasema:

> *"Dodo lenyewe limeumbwa ili liliwe na watu tunasahau hilo; sidhani kama nafsi ya dodo huridhika linapoiva likaachwa tu lianuke na kupasuka lenyewe ndipo liokotwe na kuliwa. Hizi ni dhama za mapinduzi. Tabia za kila kitu zimebadilika. Hujasikia kuwa vyura wa Kihansi wanazaa kama watu?"*

Vile vile katika tamthiliya ya *Ushuhuda wa mifupa* jamii hiyo haijui lolote juu ya madhara ya kuchomwa sindano ambazo hazijachemshwa na kuongezwa damu ambayo haijafanyiwa uchunguzi,jamii inaona kuchemsha sindano ni kupoteza muda na watu Muuguzi anambaye hajui umuhimu wa kuzichemsha hizo sindano. Mwandishi anasema:

> *"Nesi kwani ukipiga hivi hivi haziingii?" na "Sogea huko kwa manesi utoe damu ili tuweze kuokoa maisha ya mwezetu…manesi wanamtoa damu, hapo hapo Daktari anamwekea mgonjwa harafu wanamweka kando".*

Kufanana kwingine kwa waandishi hawa ni kwamba tamthiliya ya Embe dodo imetumia mbinu za ufutuhi ambazo ni mbinu ya dhihaka, kejeli, utani, ubeuzi na vijembe wakati tamthiliya ya *Ushuhuda wa mifupa* nayo imetumia mbinu zile zile za ufutuhi ambazo ni kejeli, dhihaka, utani, ubeuzi na vijembe.

### 4.3.3 Sababu za Kufanana na Kutofautiana Kwa Mbinu za Ufutuhi

Mbinu za ufutuhi katika tamthiliya za *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* zimeonekana kufanana kutokana na kwamba, tamthiliya zote zimetumia mbinu za

Ufutuhi katika kuwasilisha ujumbe ya njia za kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa Ukimwi miongoni mwa wanajamii. Pili, ujumbe uliowasilishwa katika tamthiliya zote mbili ni ujumbe wa kuelimisha jamii juu ya njia ambazo zimesababisha kuenea kwa ugonjwa wa Ukimwi katika jamii yetu na kama jamii zetu tutaziepuka hizo njia zilizowasilishwa katika tamthiliya zote mbili, basi jamii yetu itakuwa imeepukana na ugonjwa wa Ukimwi.

Mbinu hizi zimeonekana kutofautiana kutokana na kwamba tamthiliya ya *Embe dodo*, inawasilisha mila na desturi zilizopitwa na wakati kama zile za kumweka binti mwari, wanawake kutokupelekwa shule na wanaume kuwa na sauti zaidi katika jamii kuliko wanawake. Wakati katika tamthiliya *Ushuhuda wa Mifupa* kumewasilishwa ujembe wa uzembe wa serikali na jamii unavyochagia katika kueneza ugonjwa wa Ukimwi. Daktkari anamutoa damu mtu bila hata ya kupima kisha palepale anamuongeza damu mgonjwa bila hata ya kuipima damu ile kama iko salama au haikosalama.

### 4.3.4 Hitimisho

Sura hii imewasilisha na kujadili data na matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu kulingana na malengo mahususi ya utafiti kama yalivyobainishwa katika sura ya kwanza. Sura hii imebainisha mbinu za ufutuhi ambazo zimetumika katika tamthiliya zilizochunguzwa katika utafiti huu ambazo ni *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa.*Utafiti huu umebaini kuwa tamthiliya ya *Embe dodo* imetumia mbinu za ufutuhi kama vile ubeuzi,utani, kejeli, dhihaka na vijembe. Imejadiliwa katika suara hii kuwa tamthiliya ya *Embe dodo* imetumia utani na dhihaka zaidi katika

kuwasilisha maudhui ya kazi yake na hivyo kumfanya msomaji aweze kufikiri zaidi ili kuweza kubaini kile msanii alichokusudia. Wakati *Ushuhuda wa mifupa* imetumia mbinu ya kejeli zaidi ikifuatiwa na utani na dhihaka yenye lugha ya kawaida na iliyo wazi zaidi ambayo haimtaki msomaji kufikiri ili kuweza kubaini kile anachokiwasilisha msanii. Suala hii imejadili kuwa, tamthiliya hizi zinatofutiana katika kuwasilisha suala la ugonjwa wa ukimwi kwa sababu wasanii wanawasilisha historia ya jamii ya Tanzania katika vipindi viwili tofauti. *Embe dodo* anawasilisha historia ya mapambano dhidi ya ugonjwa ukimwi katika kipindi cha miaka ya 1990 hadi 2005 na hivyo kujadili juu ya historia ya harakati za kupambana na mila na desturi, mitazamo, mfumo dume ambazo zinasababisha kuenea kwa ugonjwa wa ukimwi wakati *Ushuhuda wa Mifupa* inajadili kwa uhalisia juu ya harakati za jamii katika miaka ya 1980 hadi 2000 kupambana na ujinga, umaskini, mila potofu, tamaa ya pesa ambazo zilisababisha katika kuenea zaidi kwa maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi. Kwa upande mmoja ilibainika kuwa tamthiliya hizi zimeandikwa katika kuelimisha jamii juu ya mapambano dhidi ya ugonjwa wa ukimwi ambao hauna tiba mpaka sasa.

# SURA YA TANO

# 5.0 MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Hii ni sura ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni; sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ni utafiti linganishi ambao ulilenga kutathimini mbinu za ufutuhi zilizoyumiwa na waandishi katika kuelimisha jamii kuhusu janga la ukimwi kwa kulinganisha tamthiliya ya *Embe dodo* iliyoandikwa na Dominicus Makukula na tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa iliyoandikwa* na P. Mwasanga. Lengo ni kutaka kuibua mbinu za ufutuhi ambazo zimetumika katika kuwasilisha suala la ugonjwa wa ukimwi katika jamii na kuzilinganisha kutoka kwa msanii mmoja na msanii mwingine.

Tatizo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza mbinu za ufutuhi zilivyotumika katika kuelimisha jamii juu ya ugonjwa wa ukimwi tamthiliya za ufutuhi kwa kulinganisha tamthiliya za *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* ili kuona ni jinsi gani wasanii wa tamthiliya hizo wanafanana ama kutofautiana katika uteuzi wa vipengele vya kimtindo wanapowasilisha kuielimisha jamii juu ya ugonjwa wa ukimwi. Aidha, lengo la utafiti huu kama lilivyobainishwa katika sura ya kwanza ilikuwa ni

kutathimini mbinu za ufutuhi katika kuelimisha jamii kuhusu janga la ukimwi kwa kulinganisha tamthiliya za *Ushuhuda wa Mifupa* na *Embe dodo* ili kubaini mbinu za ufutuhi zinazowafananisha na kuwatofautisha wasanii wa vitabu hivyo katika kuliwasilisha suala Elimu kwa jamii juu ya janga la ugonjwa wa Ukimwi.

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi mawili ambayo ni; Kubainisha mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* na kulinganisha na kulinganua uteuzi wa mbinu za ufutuhi katika kuwasilisha suala la Elimu kwa jamii juu ya janga la ugonjwa wa ukimwi.

Ili kufikia malengo hayo, utafiti huu ulikusudia kujibu maswali mawili ambayo ni; Ni mbinu zipi za kifutuhi zilizotumika katika *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa?* Kuna kulingana na tofauti gani katika mbinu za ufutuhi zilizoonekana katika tamthiliya ya Embe dodo na Ushuda wa Mifupa? Pamoja na kuwa kuna tafiti ambazo zimefanywa kuhusu ulinganishaji wa kazi za tamthiliya, lakini ulinganishaji huo haukuzingatia masula ya mbinu ufutuhi katika kuelimisha jamii juu ya janga la ugonjwa wa ukimwi. Vile vile tafiti nyingi zimejikita katika kulinganisha fani na maudhui ya kazi za faishi. Hivyo, bado inaonesha kuwa utafiti wa kina unahitajika ili kutafiti jinsi mbinu za ufutuhi zinavyoweza kumtofautisha msanii mmoja na msanii na mwingine katika kuelimisha jamii yetu juu ya ugonjwa wa ukimwi , pengo hili ndilo ambalo utafiti huu ulikusudia kuliziba. Ili kufikia lengo na kuziba pengo hilo, utafiti huu basi, umechunguza mbinu za ufutuhi katika tamthiliya za kifutuhi kwa kutumia mifano ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa.*

Aidha kulingana na malengo ya utafiti huu, utafiti huu ulitumia Nadharia ya Elimumitindo ambayo ilionekana inafaa na imetuongoza katika kuchunguza mbinu za ufutuhi ambazo tumezibaisha na Nadharia ya Fasihi Linganishi ambayo imetusaidia katika kubaini kufanana na kutokufanana kati ya mbinu za Ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* kisha kuchambua data za utafiti huu.

Mbinu ya usomaji wa machapisho ilikuwa ni mbinu kuu ambayo ilimsaidia mtafiti kuchambua vitabu vyote viwili na kubainisha mbinu za ufutuhi zinazotumika kujenga na kubainisha mbinu za ufutuhi zilizojitokeza.. Utafiti huu unatumia sifa za utafiti wa kitakwimu na usiokitakwimu. Aidha, data za utafiti huu zimechambuliwa kwa kutumia mbinu mbili, yaani uchambuzi bainishi na linganishi. Katika kujibu maswali ya utafiti huu, kwa kuanza na swali la kwanza, utafiti huu ulitathimini mbinu za ufutuhi katika tamthiliya ya *Embe dodo* na kubaini kuwa, msanii ametumia mbinu za ufutuhi kama vile utani, ubeuzi, dhihaka,kejeli na vijembe. Utafiti huu umegundua kuwa, msanii wa *Embe dodo* ametumia mbinu ya utani na dhihaka mara nyingi zaidi kuliko mbinu  zingine za ufutuhi na mbinu ya vijembe imetumika kwa uchache zaidi ya mbinu zote.

Aidha utafiti huu umebaini kuwa, tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* ni tamthiliya iliyotumia mbinu ya kejeli zaidi katika kujenga ya kazi yake, ikifuatiwa na mbinu ya dhihaka na utani. Utafiti huu ulibaini kuwa tamthiliya ya *Ushuhuda wa Mifupa* imejengwa kwa kutumia mbinu ya kejeli za kawaida kiasi cha kumfanya msomaji kuburudika zaidi wakati akisomo au kuisikiliza tamthiliya hii. Mbinu zingine

zilizotumika ni pamoja na ubeuzi, vjembe, utani na dhihaka. Aidha utafiti huu uligundua kuwa tamthiliya zote *Embe dodo na Ushuhuda wa Mifupa* zinawasilisha uhalisia wa historia ya kweli (mambo ya kweli yalimo katika jamii ya Tanzania).

Hivyo basi, ni vigumu sana kutoa hitimisho kuwa tamthiliya hizi zinafanana. Utafiti huu uligundua kuwa tamthiliya hizo zinafanana katika matumizi mbinu za ufutuhi ambayo ni ubeuzi, utani, kejeli, vijembe na dhihaka. Aidha, utafiti huu ulibaini kuwa tamthiliya hizi zinafanana katika katika muktadha wa utunzi wake, zote zimetungwa katika kipindi cha cha ugonjwa wa ukimwi na ndiyo maana zote zinzonesha njia zilizosababisha zaidi katika kuenea kwa ugonjwa wa ukimwi. Pia muktadha mwingine unaojitokeza ni kwamba jamii haikuwa na uelewa wa kutosha juu ya ugonjwa wa ukimwi. Athari za ugonjwa wa ukimwi na mapambano yake kwa jamii zao na kwa wasanii inawafanya watunzi wafanane.

## 5.3 Hitimisho

Utafiti huu umejadili kuwa, mbinu za ufutuhi ambazo zimetumika katika tamthiliya zilizochunguzwa katika utafiti huu ambazo ni *Embe dodo* na *Ushuhuda wa mifupa.* Utafiti huu umebaini kuwa tamthiliya ya *Embe dodo* imetumia mbinu za ufutuhi kama vile utani, ubeuzi, kejeli, vijembe na dhihaka. Utafiti huu umebaini kuwa, *Embe dodo* imetumia mbinu ya kejeli zaidi ikifuatiwa na utani na dhihaka katika kuwasilisha maudhui ya kazi yake na hivyo kumfanya msomaji aweze kufikiri zaidi ili kuweza kubaini kile msanii alichokusudia. Tofauti wakati *Ushuhuda wa Mifupa* ambayo imetumia mbinu ya kejeli zaidi ambayo haimtaki msomaji kufikiri ili kuweza kubaini kile anachokiwasilisha msanii.

Katika kuzilinganisha na kuzitofautisha tamthiliya za *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa*, tamthiliya hizi zimeandikwa katika harakati za kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi. Kwa upande mwingine ilibainika kuwa tamthiliya hizi kwa vile zimendikwa na wasanii wa jamii moja ambao wameshuhudia na kupata masimulizi ya historia ya jamii yao.Kulingana na utafiti huu, tunaweza kuona faida ya utafiti huu kwa taaluma ya fasihi na jamii kwa ujumla.

## 5.4 Mapendekezo

Kwa kutumia utafiti huu tumeweza kulinganisha tamthiliya za Ufutuhi, utafiti huu unahitimisha kuwa Tamthiliya ya *Embe dodo* na *Ushuhuda wa Mifupa* ni Tamthiliya ambazo zinatofautiana katika uteuzi na utumizi wa mbinu za ufutuhi na ubunifu wa kisanii, pia ni tamthiliya zinazowasilisha suala la kuielimisha jamii juu ya ukimwi katika nyakati mbili tofauti. Hivyo basi, utafiti huu unapendekeza kwamba ipo haja ya kufanya utafiti wa kina zaidi kuhusu kazi za tanzu zingine zilizoandikwa kuhusu ugonjwa wa ukimwi kwa jamii ikimaanisha kuwa watafiti wengi wajitokeze kufanya utafiti unaojikita katika kazi za kisanii za ufutuhi wenye maudhui ya ukimwi pia wasanii mbalimbali wajitokeze katika kutunga kazi za kifasihi zenye kubeba maudhui ya elimu juu ya kupambana na ugonjwa wa ukimwi kwani bado ni tishio kubwa kwa jamii yetu hususani katika tamthiliya ya kiswahili, pia tafiti mbalimbali zifanyike kwani zitakuza lugha na mbinu za ufutuhi, na zitasaidia wanafunzi wa Sekondari na Vyuo kutumia kazi hizo za kiutafiti kama rejea zao, pia kuwahamasisha katika kufanya utafiti. Kwa kufanya hivi tutaweza kutoa hitimisho la jinsi wasanii wanavyoweza kutumia ubunifu katika kuwasilisha suala la elimu kwa jamii katika

kupambana na ugonjwa wa ukimwi kwa kutumia mbinu za ucheshi au ufutuhi katika tamthiliya.

# MAREJELEO

Bryman, A. (2004). Social Research Methods (Toleo la 2). Oxford: UniversityPress.

Jakobson, R. (1987a). "Gremmatical parallelism and its Russian facet.Language and literature", imehaririwa na Krystyna Pomorska na Stephen Rudy. Cambridge, Mass: Beof Harvard University Press.

Jakobson, R. (1987b). "Linguistics and poetics, Language and Literature", imehaririwa na Krytyna Pomorska na Stephen Rudy. Cambridge, Mass: Belknap Press of Harvard University Press.

Jilala, H. (2003), "Giza". Daud Publishing Company, Dar es Salaam.

Jilala, H. (2016), "Misingi ya Fasihi Lingnishi. Nadharia Mbinu na Matumizi". Daud Publishing Company, Dar es Salaam.

Kezilahabi, E. (1976). "*Ushairi wa Shaaban Robert"*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Kiango, S. D. (1980). *"*Tamthiliya ya Kiswahili na Mabadiliko ya Dhamira *1957*. 1975*"* Tasnifu ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kiango, S. D. (1982). "Tamthiliya ya Kiswahili: Dhamira Chapwa na Usuli katika Uchapwa". *Jarida la Kiswahili, Isimu na Fasihi*. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Juzuu Na, 49/2 (uk: 33-56).

Kothari, C. K. (1990). Research Methods: Methods and Techniques. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, C. R. (1993). *Research Methodology": Methods and Techniques* (Toleo la 2). New Delhi: Wiley *Eastern* Ltd.

Makukula, D. Z. (2015). *Embe Dodo.* Taasisi ya Taaluma za Kiswahili Dar es Salaam.

Mapalala, B. M. (2006). *P assed like a shadow*, Dar es Salaam: DUP.

Mbogo, E. (1993). *Matumizi ya Dhana na Sanaa katika Sanaa za Maonyesho za Jadi katika Tamthiliya ya Leo.* Katika Mulokozi na Mung'ong'o (Wah).

Mbogo, E. (2015). *Nukuu ya Darasani,* Aina mbalimbali za Tamthiliya; Chuo Kikuu Huria cha Tanzan, Dar es Salaam.

Mbonde, J. P. (2002). *Uhakiki na uchambuzi wa tamthiliya*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Mdee na wenzake (2011). "Kamusi ya Karne ya 21": Kamusi ya Kiswahili yenye uketo zaidi katika karne hii, Nairobi: Longhorn Pulishers Ltd.

Medical Aid Foundation (2005). *Kilio chetu.* Dar es Salaam: TPH.

Mhando & Balisidya, (1976). *Sanaa za Maonesho na Fasihi*, Dar es Salaam: TPH.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: EAEP.

Mulokozi, M. and Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salaam: TPH.

Mulokozi, M. M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili.* Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Newmark. P. (1988). *A Textbook of Translation*. London: Prentince Hall.

Ngozi, I. (1990). "Ushuhuda wa Mifupa". Baraza la Sanaa la Taifa, Dar es Salaam.

Njogu, K & Wafura, R.M. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. & Chimerah, R. M. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi.* Nairobi: Jomokenyatta Foundation.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi.* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (2004). Fools, Drunkards, and Imbeciles Tell More Truth: Whiter Satire in Tanzania?" Katika Kiswahili, Juzuu 67, Y. M. Kihore (Mhariri), Dar es Salaam: TUKI.

Senyamanza, A. S. (H.T). *Misingi ya kazi za kubuni; Nadharia, Mbinu na Mifano ya Kazi Bunilizi*: Karljamer Print Technology.

Songoyi, (2005). Tasnifu juu ya Miundo na Maudhui ya nyimbo za Kisukuma.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* (Toleo la 2). Nairobi: Oxford University Press.

TUKI, (2013). Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Nairobi; Oxford University Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publisher.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Focus Publication Ltd. Nairobi Kenya.

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi:* Nairobi: Vide Muwa.

Wamitila, K.W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa.

Wellek, R. & Warren, A. (1996). *Theory of Literature*. Hamorndsworth: Penguin